

Iwe Nuru



"Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na nizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; wa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu" Mathayo 11:28-29

Mjifunze Kwangu

maoni yao. Mume naye alikuwa na mamlaka yote katika mambo yanayohusu jamaa yake.

Kulingana na vizazi vitatu au vinne vilivyopita, ilikuwa hivi, ikiwa mke angelizungumza na mumewe kwa ufadhili hali kuna mgeni mwanamume nyumbani kwao, mgeni huyo angeenda nyumbani kwake na kumpiga mkewe ili kumfudisha asije akamfanyia tendo kama hilo. Wanawake walichukuliwa kama wafanya kazi. Walitakiwa kufanya kazi kwa bidii. Hawakuhusishwa katika mambo ya dini.

Lakini mambo yamebadilika siku hizi. Wanawake wanapewa fursa ya kufanya mambo ambayo yalitengewa tu wanaume. Kwa mfano, jamaa nyingi zinawasomesha wasichana wao. Wanawake hawa wenye elimu wanapewa uongozi katika kazi kubwa katika jamii zetu.

Kulingana na jamii ya Kiyahudi, wanawake walichukuliwa milki ya mume na sio watu muhimu. Walitendewa tu jinsi wanawake wa Kiafrika walivyotendewa. Wanawake walikuwa na mahali pao katika hekalu na hawakutakiwa wachanganyike na wanaume. Hawakukubaliwa kutoa maoni yote.

Je! Yesu aliwatendeaje? Aliwatendea kama marafiki. Aliwaonyesha upendo. Alitaka ulimwengu ujue kwamba wanawake wana sehemu ya kutimiza katika jamii na katika ufalme wa Mungu.

Baadhi ya wanawake walisafiri na Yesu pamoja na wanafunzi wake. Mwanamke Msamaria alienda kuwashuhudia wengine baada ya kuzungumza na Yesu. Wanawake walikuwepo wakati wa kusulubishwa kwa Yesu. Wanawake walikuwa wa kwanza kumwona Yesu baada ya kufufuka.

Je! hii inatuonyesha nini sisi kama wanawake Wakristo? Tunapaswa kujua kwamba tunayo kazi ya kufanya katika kukuza ufalme wa Mungu hapa duniani. Tunapaswa kwenda na kuwaambia watu wengine habari za upendo wa Mungu. Hebu tuwaendee jirani zetu na habari njema ya wokovu. Tunapaswa kujua kwamba Mungu anatuthamini sana. Tunastahili mbele zake kupitia kwa Yesu Kristo. Wakati mambo yanapokwenda vibaya katika jamii yake, kumbuka kwamba Yesu anapenda wanawake na huwakubali jinsi anavyokubali wanaume.

KIONGOZI:

Tumejifunza katika mpango wa leo kwamba Yesu alipinga desturi zisizofaa. Tunapaswa kufuata mfano wake na kuping'a desturi mbaya na uovu katika jamii zetu. Tusimame imara kwa ajili ya Kristo. Tujaribu kuwafundisha wengine mambo ambayo Mungu anataka yatimizwe maishani mwetu. Soma Biblia yako kila wakati ili ujue yaliyo mema na ya haki na yaliyo maovu machoni pa Mungu.

IWE NURU

Waandishi: Wanawake Hawa kutoka Kenya:
Rose Kimole, Mary Waruta, Noeli Shisiali,
Grace Eyika and Beth Butler

Masoma Ya Mikutano Ya Wanawake

African Coordinated Curriculum for Women

Co-Lit 5-2-1

Published by
Baptist Publications House
Thika Road, Ruaraka
P.O. Box 30370, Nairobi

© Copyright 1992
Baptist Publications House
All rights reserved

kweli, siku hiyo haikuwa muhimu kuliko uhai. Yesu aliamua kutii amri za Mungu, hata kama ilimbidi apuuze sheria za mwanadamu.

Tunaweza kujifunza kutoka kwa Yesu kwa kujikumbusha kufanya yaliyo ya haki mbele za Mungu. Ni vyema kuwatembelea wagonjwa hospitalini na nyumbani kwao hata kama ni siku ya Jumapili. Ni vizuri kuwatembelea wazee vikongwe, kuwaletea maji, kuni, kuwafulia nguo na kuosha vyombo. Ni vizuri kwenda na kuomba pamoja nao siku ya Jumapili. Swali ambalo tunapaswa kujiuliza ni "Je! yale ninayofanya yanamtukuza Mungu?"

SEHEMU YA TATU: Aliwaonyesha Pale Walipokosea

Wambui ni mwanamke aliye heshimika sana pale Kanisani. Huwaongoza wengine katika masomo ya Biblia. Siku moja alimtembelea Mumbi, mmoja wa washiriki wa kundi lake ambaye alikuwa mgonjwa. Mumbi alikuwa mumini mpya. Mumbi aliambiwa aende nyumbani kwa sababu alishindwa kulipa gharama ya hospitalini. Wambui alipomtembelea nyumbani kwake alipata kwamba Mumbi alienda kutibiwa na mganga. Wambui hakumwambia mtu jambo hili ingawa alijua kwamba ni kosa. Lakini aliporudi nyumbani kwake, aliwaambia rafiki zake alivyofanya Mumbi na akakataa kumtembelea tena.

Yesu hakufanya hivyo wakati Mafarisayo walipo thamini sana desturi zao kuliko Neno la Mungu. Bali yeye aliwakemea papo hapo na kuwakosoa kwa kuwaambia ukweli. Wambui angemfanyia hivyo Mumbi. angemkemea kwa upendo kwa kuwa Mumbi hakuwa amekomaa Kikristo. Kisha angemfariji na kumwombea ili asamehewe na aponywe.

Yesu aliwaambia Mafarisayo yale yanayo wangojea kwa kupuuza sheria za Mungu. Yesu anaonyesha katika Luka 11:37-53 jinsi walivyopuuza haki na upendo wa Mungu. Walipenda viti vya mbele, waliwapa watu mizigo, waliwaua manabii na kukubaliana na matendo mavyu. Walikuwa kama makaburi yasiyo na alama ambayo watu waliyakanyaga bila kujua.

Mambo haya yote yapo katika makanisa yetu. Kuna watu ambao wanapenda vyeo makanisani. Wengine wanataka kutambuliwa na kuheshimiwa. Mwanamke Mkristo hapaswi kujitakia mambo haya. Anapaswa kunyenyekea mbele za Mungu naye atakwezwa. Tunapaswa kuwakemea na kuwakosoa watu kama hawa kwa ukweli na upendo badala ya kuwaacha waendele katika dhambi.

SEHEMU YA NNE: Uhusiano wa Yesu na Wanawake.

Kulingana na desturi za Kiafrika wanawake hawakuthaminiwa sana katika jamii zetu. Walichukuliwa kama watoto. Hawakukubaliwa kutoa

watoto. Wazazi wao walijitolea kulipa gharama ya uganga. Lakini Juliet na Ngugi walikataa. Wao wanamngojea Mungu awabariki na mtoto.

Jamaa hii walifanya jambo jema mbele za Bwana. Walikataa kumwasi Mungu hata ingawa walihitaji sana mtoto. Waliadini na kumtii Mungu hata wakati ambapo hawakukubaliana na wazazi wao.

Tutajadiliana katika mpango wa leo jinsi Yesu alivyopinga desturi zisizofaa. Hii itatusaidia kujua jinsi ya kupinga na kuepuka desturi na mafundisho yasiyofaa katika jamii yetu.

SEHEMU YA KWANZA: Yesu Alikariri na Kueleza Maandiko

Njia moja ambayo Yesu alipinga desturi zisizofaa ni kwa kukariri Maandiko. Luka 6:3-5, 1 Samweli 21:1-6. Mafarisayo walimwuliza Yesu kwa nini wanafunzi walikuwa wakivunja na kula masuke siku ya sabato. Yesu aliwakumbusha jinsi Daudi na askari wake walivyokula mkate katika nyumba ya Mungu wakati walipokuwa wakimtoroka Sauli. Mkate huu ulitakiwa kuliwa na makuhani peke yao. Lakini Daudi na askari wake walikula, nao hawakuadhibiwa na Mungu. Daudi alimpenda Mungu kwa moyo wake wote na alimtegemea kwa kila jambo. Yesu aliwaambia Mafarisayo kwamba lililo muhimu ni kumwabudu Mungu kwa moyo wako wote, wala siyo siku ya kuabudu.

Yesu alieleza kwamba yeye ndiye Bwana wa Sabato. Ni vizuri kufanya yale yanayompendeza Mungu siku ya sabato. Aliwakumbusha kwamba wao wangemtoa kondoo wao shimoni ikiwa angeanguka humo siku ya sabato. Kwa hivyo ilikuwa muhimu zaidi kwake kuponya siku ya sabato.

Ni lazima sisi kama wanawake Wakristo tujue yale ambayo Biblia inafundisha. Kisha tutajua jinsi ya kutatua mambo ya jamii yetu yanayokwenda kinyume cha mafundisho ya neno la Mungu. Biblia itatusaidia kufanya hivyo. 2 Timotheo 3:16 inasema, "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki." Tunapaswa kufanya yaliyo ya haki mbele za Mungu kuliko mbele za wanadamu.

SEHEMU YA PILI: Yesu Aliuliza Maswali Yanayofaa

Njia nyingine ambayo Yesu alipinga desturi zisizofaa ni kwa kuuliza maswali. Alitaka Mafarisayo wafikirie juu ya desturi zao na wabadili nia zao mbaya. Yesu aliwauliza Mafarisayo katika Luka 6:9 kwamba, "Je! ni halali siku ya sabato kutenda mema, au kutenda mabaya? Kuponya roho au kuangamiza?"

Yesu alitumia swali hili kuwaonyesha jinsi walivyo sahau sheria. Walipuuza amri za Mungu na kutii sheria za mwanadamu. Kwa

IWE NURU

YALIYOMO

MJIFUNZE KWANGU

Mpango 1 - Yesu Mwalimu Wetu	5
Waandishi: Noel Shisiali, Grace Eyika na Beth Butler	
Mpango 2 - Huruma	7
Mwandishi: Mary Waruta	
Mpango 3 - Bwana, Tufundishe Kuomba	11
Mwandishi: Beth Butler	
Mpango 4 - Jinsi ya Kushughulikia Majaribu	14
Mwandishi: Rose Kimole	
Mpango 5 - Uhusiano wa Yesu na Watu	18
Mwandishi: Rose Kimole	
Mpango 6 - Upendo	21
Mwandishi: Rose Kimole	
Mpango 7 - Majivuno na Unyenyekevu	26
Mwandishi: Rose Kimole	
Mpango 8 - Imani na Kuamini	30
Mwandishi: Rose Kimole	
Mpango 9 - Kuwaambia Wengine Habari Njema	33
Mwandishi: Beth Butler	
Mpango 10 - Yesu na Desturi	36
Mwandishi: Rose Kimole	
Mpango 11 - Desturi na Amri za Mungu	39
Mwandishi: Rose Kimole	
Mpango 12 - Jinsi Yesu Alivyopinga Desturi Mbaya	41
Mwandishi: Rose Kimole	

Co-Lit 5-2-1

asimwache. Na mwanamke, ambaye ana mume asiyeamini, na mume huyo anakubali kukaa naye, asimwache mumewe...kwa maana wajuaje, wewe mwanamke, kama utamwoko mumeo? au wajuaje, wewe mwanaume kama utamwoko mkeo?" (1 Wakorintho 7:12-16).

Ni vyema kwetu sisi wanawake Wakristo kusoma na kujifunza Biblia yote na kumwomba Mungu atufunulie ukweli. Yesu alisema kwamba, "Tena mataifahamu kweli, nayo kweli itawaweka huru," (Yohana 8:32.)

Dini zingine zimeifanya imani ya kikabila kuchukua mahali pa Biblia. Kwa hiyo, Biblia haina mamlaka kwao jinsi inavyotakikana. Bali wanaongozwa na ndoto, maono na

roho tofauti. Hebu tujihadhari na tujifunze kutoka kwa Kristo, ili tusipatikane kuwa mashahidi wa uongo na waalimu waongo wa Neno la Mungu.

KIONGOZI:

Tumwombe Mungu atusaidie kutokuwa kama Mafarisayo ambao waliwatwika watu mizigo ya sheria walizojitungia ambazo wao wenyewe hawakuzitii. Tunapaswa pia kushtumu mafundisho yasiyo ya kweli yaliyo katika makanisa yetu na tufundishe ukweli wa Biblia kama Yesu. Tumwombe mchungaji wetu na viongozi wengine wa dini mbalimbali, kwamba wataweza kujifunza, kufundisha na kuelewa vizuri Biblia.

Mpango wa Kumi na Mbili

JINSI YESU ALIVYOPINGA DESTURI MBAYA

Kilini Cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatiifu: Luka 6:1-11; 13:10-17

Kifungu Cha Kukumbuka: "Petro na Yohana wakawajibu wakawaambia, kwamba ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe." Matendo 4:19

KIONGOZI:

Juliet ameolewa na Ngugi. Wote ni Wakristo waaminifu. Bado hawajapata mtoto baada ya kuoana kwa miaka kumi. Wanaamini kwamba watoto ni zawadi kutoka kwa Mungu kwa hivyo wote

wametosheka na hali hii ambayo Mungu amewapatia.

Wazazi wa Juliet na Ngugi hawajaokoka. Wao na wana kijiji wengine wanawataka Juliet na Ngugi wamwendee mganga ambaye amewasaidia jamaa zingine kupata

watu ambao Isaya aliandika juu yao, "Watu hawa huniheshimu kwa midomo; ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu." (Mathayo 15:2,3,8-9).

Yesu aliwaambia wazi wao na sisi kwamba amri za Mungu ni muhimu zaidi kwetu kuliko desturi zetu. Hatupaswi kuvunja amri za Mungu ili tufuate desturi zetu.

SEHEMU YA PILI: Desturi za Kanisa Ambazo Haziambatani na Mafundisho ya Biblia.

Ifuatayo ni hadithi ya kweli iliyotokea miaka michache iliyopita. Majina siyo ya wahusika lakini habari yenyewe ni ya kweli.

Jirani yake wanjiru alimshuhudia habari za Yesu Kristo. Wanjiru alimua kumpokea, Yesu kama Mwokozi wake. Kisha alimwambia bwanake Kamau. Kamau alifurahi sana kusikia kuwa mke wake atabadili maisha yake ya dhambi. Kamau hakuwa ameokoka, lakini alimwambia mkewe waende katika kanisa fulani. Walienda kuzungumza na mchungaji baada ya ibada kuisha.

Mchungaji aliwaambia sheria za kanisa walipoendelea kuzungumza. Wanjiru hakutakiwa kusuka nywele zake. Ni lazima avae nguo ndefu na kujifunga kitambaa cheupe kichwani. Hapaswi kuvaa nguo za bei ghali, ushanga au bangili. Kamau naye alitakiwa kufunga kilemba kichwani. Kamau alipoulizwa ikiwa anataka

kuokoka, alijibu kwamba hayuko tayari. Alivunjwa moyo na masharti aliyopewa na mchungaji.

Mchungaji aliwaambia kwamba ikiwa Kamau amekataa kuokoka, basi Wanjiru hawezi kuokoka kwa sababu hatakubaliwa kuishi na bwana ambaye hajaokoka. Kama anataka kuokoka peke yake, basi ni lazima amwache mumewe. Mchungaji huyo alikariri vibaya Biblia kwa kusema kwamba ni lazima wokovu ukubalike na jamaa yote.

Wanjiru hakuwa na la kufanya. Hata aliambiwa pia kwamba mwanamke aliyemshuhudia alikuwa mwenye dhambi kwa sababu wanawake hawaruhusiwi kuhubiri. Wanjiru alimwamini mchungaji huyo na akaamua sasa hana haja ya kuokoka. Wanjiru hajaokoka hadi wa leo.

SEHEMU YA TATU: Desturi Katika Kanisa

Hadithi ambayo tumeambiwa inatuonyesha jinsi Wakristo wanavyoweza kuchanganyikiwa. Mambo yote ambayo Wanjiru aliambiwa hayana uhusiano na wokovu. Biblia inasema tu kwamba, "Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka," (Matendo 16:31).

Pia, hakuna mahali po pote katika Biblia panaposema kwamba mke au mume hawezi kumpokea Kristo ikiwa wote wawili hawampokei. Ila Paulo anasema kwamba, "Iwapo ndugu mmoja ana mke asiye amini na mke huyo anakubali kukaa naye

YESU MWALIMU WETU

Kilini cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatifu: Mathayo 11:28-30

Kifungu Cha Kukumbuka: "Jilieni nira yangu, mjifunze kwangu, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsiini mwenu."

Mathayo 11:29

KIONGOZI:

Tutaanza leo mfululizo wa masomo kuhusu Yesu Mwalimu wetu. Hebu tusome tena maandiko yetu ya leo: "Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mzigo, nami nitawapumzisha. Jilieni nira yangu mjifunze kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsiini mwenu, kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi." (Mathayo 11:28-30).

Jina ambalo wanafunzi walitumia sana kumwita Yesu ni "Mwalimu." Ikiwa tunataka kujifunza kuishi maisha ya Kikristo, hakuna mtu mwingine wa kujifunza kwake isipokuwa Yesu. Tutajifunza katika masomo haya jinsi Yesu alivyo watendea watu na kusuluhisha matatizo. Tutaona jinsi Yesu alivyofuata Mungu kwa kila jambo.

Tuanze leo kuomba kwamba tutafanya kama Yesu tunapooni mifano yake. Tuyashike maneno ya Yesu yaliyo katika kifungu cha

kukumbuka cha leo: "Mjifunze Kwangu."

SEHEMU YA KWANZA:
Asumbukae na Wenye Kulemewa.

Je! mwili wako utajisikiaje ikiwa utafanya kazi kwa mwezi mzima bila kupumzika? Je utahitaji nini? Sote twajua kwamba mtu kama huyu atakuwa mchovu sana na atahitaji kupumzisha akili na mwili wake.

Yesu alijua kwamba watu wanasumbuka mioyoni mwao. Walisumbuka maishani mwao. Hawakujua kitakacho fanyika baadaye. Walihofia chakula, kinywaji na mavazi. Walisumbukia vitu ambavyo wangeona, na kuhisi na kushika. Walifikiri kwamba watapumzika wakivipata. Kuna watu siku hizi wanaofikiri kwamba hawatapata shida ikiwa wao ni matajiri. Lakini shida ya mwanadamu ni zaidi ya mambo ya kimwili. Yesu aliuona umati uliomfuata wakiwa wamechoka kiroho. Aliwaahidi pumziko la roho zao.

Bila shaka watu hao walishangaa kwa nini Yesu anawaambia "Njoni

kwangu" wakati wao wenyewe wako pamoja naye. Hata pengine nasi tunashangaa pia. Ni lazima tutambue kwamba Yesu alikuwa haiti miili yao bali roho zao. Yesu anataka tujivike nira yake. Hii ina maana kwamba tuungane naye kufanya kazi aliyopewa na Baba yake. Tunapaswa kuwaambia wengine habari za Yesu Mwokozi.

Yesu alitupa mfano wa kufuata. Hii ina maana kwamba ni lazima tujifunze kwake. Yesu alifanyika mwanadamu na kuishi kama sisi. Alisikia njaa, kiu, alipigwa, alijaribiwa na kudharauliwa. Alikuwa mtulivu na mnyenyekevu na aliomba kila wakati. Alijua kwamba Mungu ni mkuu kuliko shida alizopata. Alipata utulivu na amani katika Mungu.

SEHEMU YA PILI: Yesu Aliahidi Pumzike

Yesu aliiangalia mioyo ya watu na kuona kwamba wamebeba mizigo mizito ya dhambi maishani mwao. Hawakuwa na amani wala furaha mioyoni mwao kwa kusumbuliwa na vitu vya ulimwengu huu. Yesu aliwaahidi pumziko wale ambao wangeitikia mwito wake wa kuwa watoto wake. Aliwaahidi pumziko wale wasumbukao na wenye kulemewa na mizigo mizito.

Pumziko si kwamba kutofanya kazi, au kutopata shida na mateso. Pumziko ni kutokuwa na hatia, wasiwasi, mashaka na kutofahamu maana. Yesu anaahidi maana ya maisha, tumaini. hakikisho, amani na

furaha. Hata tuwapo na shida tunaweza kuvumilia kwa sababu yuko pamoja nasi. Kumfuata Yesu huleta matumaini ya kuishi katika upendo wake.

Mwanamke mmoja alitembea kando ya barabara akiwa na mzigo mzito kichwani. Alikuwa amechoka sana. Punde gari lilifika na kusimama. Lakini mwanamke huyu hakutua mzigo wake alipopanda gari hilo. Hakukaa chini. Aliendelea kusimama na mzigo wake kichwani. Dereva alimsihi akac chini lakini alikataa. Mwishowe dereva huyo alisimamisha gari na kufungua mlango. "Nilitaka kukusaidia ili upumzike," akamwambia. "Lakini umekataa msaada wangu. Chukua mzigo wako na ujiende mwenyewe."

Hadithi hii ni ya kuchekesha, lakini watu wengi ni kama mwanamke huyu. Yesu amejitoa ili atupumzishe. Lakini huwa tunakataa kumpa shida na mizigo yetu. Je! unafanya kama mwanamke huyu aliyebebwa na gari? Au umekwisha mpa Yesu mizigo yako?

SEHEMU YA TATU: Jinsi Yesu Alivyofundisha Watu:

Yesu alikuwa mwalimu. Hakufundisha darasani, bali alifundisha kwa maisha yake. Alifundisha po pote alipokwenda. Alifundisha mara nyingi umati mkubwa wa watu. Watu walifurahi sana kumsikiliza kwa sababu alifundisha kwa mamlaka makuu, na siyo kama waalimu wengine. Watu

mwetu? Kwa nini? (Wanawake watatoa sababu kama: kuhudhuria kanisa, Meza ya Bwana, Ubatizo,

zaka, fungu la kumi, kufunga na kadhalika)

Mpango wa Kumi Na Moja

DESTURI NA AMRI ZA MUNGU

Kilini Cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatifu: Mathayo 15:1-20

Kifungu Cha Kukumbuka: "Sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa Bwana ni amini, humtia mjinga hekima." Zaburi 19:7

KIONGOZI:

Desturi nyingi zinaweza kupatikana makanisani. Baadhi yazo ni nzuri na hutukumbusha wema wa Mungu na jinsi alivyotusaidia maishani. Zingine ni Sheria za ziada kama zile za Mafarisayo. Haziwezi kutusaidia katika maisha yetu ya Kikristo, bali ni mzigo kwetu. Waumini wa kundi fulani wanaweza kusisitiza kifungu fulani na wapuuze mafundisho ya Biblia. Kwa mfano, baadhi ya waumini husema kwamba kama huneni kwa lugha, basi kuna shida katika maisha yako ya Kikristo. Wengine husisitiza kwamba ni lazima uvae mavazi aina fulani na kula vyakula fulani. Lakini sisi kama wanawake Wakristo tunapaswa kujua mema na mabaya. Mungu atatuonyesha mema na mabaya tunaposoma Neno lake lote na kutafuta uongozi wake.

SEHEMU YA KWANZA: Yesu Mfano Wetu

Yesu alifuata amri za Mungu wakati desturi za Kiyahudi zilipotofautiana na sheria za Mungu. Alimfanya Mungu kuwa wa kwanza. Alijua kwamba baadhi ya desturi za Wayahudi zilikuwa mzigo kwa watu. Zingine zilikuwa za kuwatukuza kama kuwapigia saluti wakiwa, sokoni.

Tunamwona Yesu, katika Mathayo 15 akikosoa baadhi ya desturi mbaya za Kiyahudi. Mfarisayo waliwaona wanafunzi wa Yesu wakila kabla ya kunawa mikono yao. Wakauliza, "Mbona wanafunzi wako huyahalifu mapokeo ya wazee?"

Yesu akawajibu, "Mbona ninyi nanyi hualifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?" Alisema kwamba sheria walizojitungia zilikuwa muhimu sana kwao kuliko Neno la Mungu. Walikuwa kama

waondoke Misri. Kila jamaa ya Kiyahudi walitakiwa kumwua mwana kondoo na kupaka damu yake kwenye vizingiti vya mlango. Kisha walikula nyama yenyewe baada ya kuipika kwa njia fulani. Wakati malaika wa mauti alipopita katika nchi hiyo usiku huo, alipita bila kudhuru nyumba zilizopakwa damu.

Mungu aliwaamuru Wayahudi washerehekee pasaka kila mwaka kwa sababu alitaka wakumbuke jinsi alivyo waokoa. Walipika na kula nyama ya mwana-kondoo. Wazazi waliwaambia watoto wao kuhusu malaika wa mauti. Waliwafundisha jinsi Mungu alivyowalinda Waisraeli. Desturi hii ilikuwa njia ya kuwasaidia watu kukumbuka nguvu za Mungu na pia kuwafundisha watoto wao.

Yesu alipokuwa na miaka kumi na miwili alienda na wazazi wake Yerusalemu kusherehekea pasaka. Hatimaye aliendelea kusherehekea kila mwaka. Yesu hakujaribu kubadili desturi hii kwa sababu ilikuwa nzuri. Iliwakumbusha watu jinsi Mungu alivyo waokoa kutoka utumwani.

SEHEMU YA NNE: Yesu na Sabato

"Nafikiri kwamba leo nitaombea nyumbani. Mungu yuko kila mahali. Nitaombea tu hapa badala ya kwenda kanisani kwa sababu nina kazi nyingi," Maria alisema hivyo Jumapili moja.

Wakristo wengi huwa na tabia ya kutokwenda kanisani kama Maria. Ni kweli kwamba Mungu yuko kila

mahali. Lakini, Je! Yesu alitufundisha nini juu ya kukutana na waumini wengine?

Yesu alihudhuria Sinagogi kila Jumamosi. Siku ya kuabudu ya Wayahudi. Alijua kwamba ni muhimu kuwa na ushirika na watu wa Mungu. Alifuata yale ambayo Mungu aliwaagiza Waisraeli, "Ikumbuke siku ya sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni sabato ya Bwana, Mungu wako. Siku hiyo usifanye kazi yo yote" (Kutoka 20:8-10). Wazazi wake walipompata hekaluni baada ya kupotea kwa siku tatu aliwaambia, "Kwa nini kunitafuta? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?" (Luka 2:49).

Ni lazima sisi kama wanawake Wakristo tutambue umuhimu wa desturi ya kukutana pamoja kama waamini. Ni lazima tuwafundishe watoto wetu thamani ya kwenda kanisani kila wakati.

KIONGOZI:

Kuna mambo mengine ambayo Yesu alifanya yanayo ambatana na desturi za siku zake. Alifuata zile zilizotimiza amri za Mungu. Yesu alifurahia kufanya mapenzi ya Mungu. Tujifunze kutoka kwake na tutamani kufanya yale ambayo yatampendeza Mungu. Hebu tuchukuwe dakika chache kuorodhesha baadhi ya desturi za kikristo. Je! tunafuata desturi hizi maishani mwetu na makanisani

wengi walienda kumsikiliza alipokuwa katika eneo lao. Yesu alifundisha, na mara mbili aliwalisha watu wapatao elfu nne, wanawake pamoja na watoto.

Yesu alifundisha wanafunzi wake. Walikuwepo kila wakati Yesu alipofundisha umati, lakini pia alikuwa nao peke yao. Wakati mwingine wanafunzi wake wangemwendea na kumwuliza mambo ambayo hawakuelewa. Yesu aliwaelezea tena kila kitu. Yesu anataka tumwendee na maswali yetu.

Yesu aliwafundisha watu katika nyumba zao. Aliwatembelea mafarisayo, watoza ushuru na wengine. Aliwatembelea marafiki zake. Hasa alipendelea sana kuwatembelea Maria, Martha na Lazaro. Aliwafundisha alipokuwa huko. Tunapaswa kuwa tayari kumwalika Yesu kufundisha manyumbani mwetu.

Yesu alifundisha katika sinagogi, kanisa la Kiyahudi. Alienda katika sinagogi kila Jumamosi, siku ya kuabudu ya Wayahudi. Alijua kwamba watu wataenda huko kujifunza habari za Mungu. Siku hizi tunaweza kukutana na Yesu kila Jumapili kwa kujifunza Biblia na Wakristo wengine. Tunapaswa kuhudhuria masomo ya Biblia na Wakristo wengine. Natuchukue nafasi hii yakujifunza Biblia kwa watu wazima na pia ibada ikiwa tunataka kujifunza kutoka kwa Yesu.

KIONGOZI:

Tumesikia leo jinsi Yesu alivyokuwa mwalimu. Anataka tujifunze kwake. Tutakuwa tukisikia habari za Yesu katika masomo haya. Tutaona jinsi alivyoishi kama alivyofundisha. Tunaweza kuishi maisha anayotufundisha Yesu kwa kusaidiwa tu na Roho Mtakatifu. Tujitoe leo kujifunza kutoka kwa Yesu na tutende jinsi tunavyojifunza.

Mpango wa Pili

HURUMA

Kiini cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatifu: Mathayo 15:29-31

Kifungu cha Kukumbuka: "Na kila mfanyalo, kwa neno na kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye."

Wakolosai 3:17

KIONGOZI: Kiini chetu cha leo kinahusu Yesu kama Mwalimu.

Tunataka tujifunze jinsi Yesu alivyokuwa mwenye huruma.

Tunaamini na kutumai kwamba tutafuata mfano wa Yesu kwa nguvu za Mungu. Tumwombe Mungu ajidhihirishe kwetu tunapojifunza somo hili.

SEHEMU YA KWANZA: Yesu Alionyesha Huruma Kwa Kuulilia Mji wa Yerusalemu

Watu walihitaji sana kiongozi mwaminifu katika wakati huu wa historia kuliko wakati mwingine wote. Watu wanahitaji sana uongozi. Lakini huchanganyikiwa wanaposikia watu wakihubiri dini na makundi mbalimbali. Ukiwa katika mji wowote mkubwa wakati wa chakula cha mchana utaona watu wakirandaranda kama kondoo waliopotea wanaotafuta mchungaji. Watu wengi wana shida ya ukosefu wa kazi, umaskini, watoto wakaidi na jamaa zilizotengana. Wanahitaji mtu ambaye wataamini na ambaye atawapa matumaini.

Kama Yesu angekuwa duniani sasa, angeililia miji yetu jinsi alivyo ulilia mji wa Yerusalemu. Tunaambiwa katika Luka 19 jinsi Yesu alivyolia baada ya kuukaribia mji wa Yerusalemu kwa sababu ya kukataliwa na watu. Akasema, "Laiti ungalijua, hata wewe katika siku hii, yapasayo amani! Lakini sasa yamefichwa machoni pako."

Sisi kama ushirika wa wanawake, tunaweza kupanga kwenda na kushuhudia watu wa jamii yetu. Tunaweza kuwaendea wenye

mahitaji. Tunapaswa kuomba ili tuwe chumvi na nuru ya ulimwengu.

Wakati mwingine wanawake Wakristo huhitaji msaada ili waweze kusaidia wengine. Pengine tunaweza kuwaalika wataalamu kama madaktari wauguzi, au wafanya kazi wa jamii kuja na kutufundisha. Nasi tutakuwa katika hali nzuri ya kuweza kuwasaidia wengine.

SEHEMU YA PILI: Yesu Alionyesha Huruma Kwa Kuwalisha Watu

Ni jambo la kututia moyo sisi Wakristo kujua kwamba Yesu aliwajali wenye njaa. Hakuja tu kushughulikia hali yetu ya kiroho. Baadhi ya wahubiri wa siku hizi hujaribu kupuuza mahitaji ya kimwili ya watu wengine. Yesu alituonyesha mfano mzuri. Hatuwezi kufanya miujiza kama ya Yesu, lakini tunaweza kusaidia kwa kutumia kile ambacho Mungu ametupatia. Yesu hakupuuza mahitaji ya wanadamu. Aliwahurumia wenye njaa na kuwalisha. Ni jambo la kushangaza kwamba sisi tulio wanadamu hatuwahurumii wenye njaa.

Je, ni funzo gani ambalo sisi wanawake Wakristo tunaishi katika Afrika iliyo na njaa tunaweza kujifunza kutoka kwa Yesu? Ni rahisi kupuuza wazo la kuwalisha watu wenye njaa hapa Afrika. Kuna watu wengi walio na njaa ambapo hatujui jinsi ya kuwasaidia.

Kuna maskini waombaji kwenye miji yetu. Mpaka tunashindwa tumpatie nani. Wanawake Wakristo

hizi zilifanywa kuwa desturi baada ya kufuatwa na kizazi baada ya kizazi.

Wayahudi hawakufuata tu sheria za Mungu, walianzisha pia desturi zao. Baadhi ya desturi hizi hazikuhitajika maishani. Baadhi yazo zilichukua mahali pa sheria walizopewa na Mungu. Sheria hizi za kujiongezea zilifikia karibu mia nane wakati ambapo Yesu aliishi. Sheria hizi za ziada zilikuwa mzigo mzito kwa watu. Hii ndiyo sababu Yesu aliwaambia watu, "Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jilieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mweni; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi," (Mathayo 11:28-30).

Yesu aliwahurumia watu kwa sababu wana sheria waliongezea visheria vingi ambavyo watu hawakuweza kutii. Yesu hakuja kuharibu desturi za Waisraeli. Alikuwa kutimiza mafundisho ya manabii.

SEHEMU YA PILI: Desturi Katika Jamii Zetu

Sisi, kama Wayahudi, tunazo desturi ambazo tumeachiwa na vizazi vyetu. Baadhi ya desturi hizi ni nzuri na zamuhimu maishani, kama kuwaheshimu wazazi na watu wazima. Zingine hazifai. Mwanamke Mkristo anapaswa kujihadhari ili kufuata njia za Mungu badala ya njia

za mwanadamu. Shida hutokea mara kwa mara tunapoiga desturi na mila za watu wengine. Mfano mzuri ni kuiga mtindo wa mavazi ya Kizungu.

Shida kubwa tuliyonayo ni ile ya kuchanganya desturi na mila za kiasili na imani za Kikristo. Kwa mfano, ilikuwa vyema kwa wanaume kunywa pombe wakati wa arusi. Lakini Biblia inatuambia kwamba pombe ni mbaya. Badala ya pombe, tunaambiwa tujazwe na Roho wa Mungu. Siku hizi watu huona kanisani. Kisha hupanga sherehe nyingine baada ya kutoka kanisani ambako watakula na kunywa usiku kucha. Harusi hiyo inaanza vizuri lakini inaisha kinyume cha mapenzi ya Mungu.

Kristo hatukuzwi katika tendo hilo. Anasema hatuwezi kutumikia mabwana wawili. Hatuwezi kumtumikia Mungu na shetani wakati mmoja. Sisi kama wanawake Wakristo tunastahili kuwasaidia vijana na wasichana wetu. Tunaweza kuwasaidia kuona mambo yanayofanywa katika harusi za kinyumbani ambayo ni mema na kuyafanya katika arusi zinazofungwa kanisani. Wakristo hawapaswi kufuata desturi ambazo zinavunja amri za Mungu.

SEHEMU YA TATU: Yesu na Pasaka

Wayahudi walisherhekea pasaka mara moja kwa mwaka. Ulikuwa wakati ambapo walikumbuka jinsi Mungu alivyo mshawishi Farao awaruhusu wana wa Israeli

hatua ya kwenda kushuhudia? Je! tuko tayari kusema na watu ambao tunajua ni "wenye dhambi." Je! tuko tayari kuzungumza na watu wa kabila au taifa lingine na kuwaambia upendo wa Mungu?

Chukueni dakika chache na mpange jinsi kundi lenu la wanawake

Mpango wa Kumi

YESU NA DESTURI

Kilini Cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatiifu: Mathayo 15:1-20

Kifungu Cha Kukumbuka: "Akajibu akawaambia, Mbona ninyi nanyi huialifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?" Mathayo 15:3

KIONGOZI:

Je! desturi ni nini? Je! desturi ni nzuri au ni mbaya? Je! Mungu anakubali desturi zetu?

Desturi inaweza kuwa mapokeo kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Tunaweza kuwa imani mazoea yanayofuatwa na jamii. Ni kitu cho chote kinacho elezea mataifa ya jamii au kabila.

Baadhi ya desturi ni nzuri na zingine hazihitajiki maishani. Mungu hukubali desturi ambazo ni nzuri. Lakini hakubali wala kuruhusu zile ambazo ni kinyume cha amri zake.

Tutaona katika mpango wa leo jinsi Yesu alivyo shughulikia desturi za wakati wake. Alifuata zile ambazo

mtakavyoenda kushuhudia pamoja. Pengine mtapanga kwenda wawili wawili au watatu watatu. Mfikirieni mtu ambaye anataka kusikia habari za Yesu. Je! utamwambiaje habari hii? Mwombee mtu huyo na mpange kwenda kuzungumza naye.

ziliambatana na utimizaji wa mpango wa Mungu.

SEHEMU YA KWANZA: Yesu na Desturi

Yesu alizaliwa katika jamii ya Kiyahudi. Wayahudi walikuwa na desturi zao. Baadhi ya desturi hizi zilikuwa nzuri na zingine hazikufaa kamwe.

Tunajua kulingana na Biblia kwamba Wayahudi walikuwa taifa teule la Mungu. Walipaswa kuonyesha ulimwengu kwamba kuna Mungu aliye hai anaye tawala mbingu na nchi. Mungu aliwapa Wayahudi sheria na maagizo ambayo walipaswa kufuata. Sheria hizi ziliwafundisha kuhusu uhusiano wao na Mungu, na watu wengine na jinsi ya kufundisha watoto wao. Sheria

wanapaswa kumwomba Mungu awape moyo wa kutaka kuwasaidia wenye njaa wakati mwingine huwa tunafikiri kwamba sisi tu maskini sana wa kutoweza kuwasaidia wengine. Tunapaswa kuamini kwamba Mungu atatupa chakula cha kutosha na hata tubaki na cha kuwapatia wengine.

Mwanamke mmoja aliyeishi Nairobi aliwahirumia watoto wenye njaa waliokaa katika barabara za mji huu. Alianza kuwaalika nyumbani kwake na kuwapa chakula. Wengine walianza kuishi naye. Mwishowe alipewa kiwanja na akaanzisha makao ya watoto yatima. Wakristo wengi wamempa pesa za kusaidia kudumisha kazi yake. Sisi kama wanawake Wakristo tunaweza kusaidia makao kama haya kwa pesa, nguo, chakula na vitu vingine. Wanawake Wakristo wanaweza kupanga na kanisa kuwalisha watu ikiwa kanisa lao liko katika jamii ya maskini.

SEHEMU YA TATU: Yesu
Alionyesha Huruma Kwa Kuwaponya watu

Kuna magonjwa aina mbali mbali hapa Afrika. Huwa tunatamani Yesu aje na atembee katika vijiji vyetu, miji na hospitalini akiwaponya wagonjwa. Huwa tunafarijika kujua kwamba Yesu anajua shida zetu na anatumia. Yesu angali anaendelea na huduma yake ya kuponya lakini kwa njia tofauti. Ombi la mwanamke Mkristo lapaswa kuwa kwamba ajazwe na huruma kama Yesu. Nia

ya kuwatunza wagonjwa inaweza kuwa dawa kwa baadhi ya wazazi.

Wakristo na wasio Wakristo wanajua jinsi ya kuwapeleka wagonjwa hospitalini. Je! ni njia zipi zingine ambazo wanawake Wakristo wanapaswa kufuata kwa kuwatunza wagonjwa? Kusoma Neno la Mungu, kuomba na kuwatia moyo kunaweza kuwa dawa nzuri kwa wagonjwa. Maneno tunayotumia yanaweza kutibu wagonjwa. Mtu mmoja aliyetembelea hospitali alimwambia mgonjwa kwamba, "Ulikuwa njiani ukielekea mbinguni." Mgonjwa huyo hakufurahia maneno haya. Ni lazima wanawake Wakristo wajihadhari na maneno wanayotumia. Wajibu wetu kama Wakristo ni kuwabariki wale tunaokutana nao.

Wanawake Wakristo wanaweza kufanya mambo ya kuwavutia wagonjwa. Ni jambo muhimu kuwatembelea wagonjwa nyumbani kwao na hospitalini. Wanawake Wakristo huonekana mara kwa mara wakiwa na shughuli nyingi za kutoweza kutimiza kazi hii. Shughuli kuu ya Yesu ilikatizwa na Bartimayo kipofu katika Marko 10:46-52. Watu wengi walijaribu kumnyamazisha Bartimayo na kumkatiza asimsumbue Yesu. Lakini Yesu alisimama na akamponya. Ni lazima tutumie baadhi ya wakati wetu wa shughuli kuu kuwatunza wagonjwa.

Pengine tunaweza kutoa mchango wa chakula, pesa au msaada mwingine. Wanawake Wabatisti wanaweza kujiunga kama kundi na

kurwatembelea wagonjwa, hasa wale waliolazwa. Ushirika mmoja umepanga kwenda kutembelea na kula pamoja na wagonjwa waliolazwa wa kanisa kila mwaka wakati wa Krismasi. Tendo hili huifanya Krismasi kuwa ya maana kwa mgonjwa huyo.

SEHEMU YA NNE: Yesu Alionyesha Huruma Kwa Kuwabariki Watoto

Yesu aliwashughulikia watu wote. Hakuwapuza watoto. Aliwahakikishia kwamba wanayo nafasi katika ufalme wa Mungu. Alisema kwamba ufalme wa Mungu ni kwa wale ambao wana imani kama ya watoto.

Je! tunawezaje kuwabariki watoto? Tunaweza kuwabariki ikiwa tayari Bwana ametubariki. Wanawake Wakristo wanapaswa kushughulikia mambo ya kiroho na kimwili wa watoto. Tunapaswa kuwafundisha Neno la Mungu na kuomba nao manyumbani mwetu na kuonanisani.

Sisi Waafrika wakati huu tunapaswa kuguswa na hali ya watoto. Kunao watoto wengi ambao wameachwa. Tunahuzunishwa na hadithi katika magazeti za watoto walichomwa au kupigwa hadi kufa. Wakati mwingine hatuwezi kusaidia lakini uovu huu huwagusa sana wanawake.

Hatuwezi kuondoa taabu na dhiki yote, lakini tunaweza kujaribu kuwa chumvi na nuru katika eneo tunaloishi. Nia tabia na matendo yetu

yaweza kuwaathiri watoto. Wanawake Wakristo wanaweza kupanga kuwa na semina juu ya watoto na wajibu wa wazazi. Watoto maskini na yatima wanaweza kuhudumiwa jinsi tulivyo ambiwa katika Sehemu ya Pili. Watoto wanahitaji kuhakikishiwa upendo wetu na upendo wa Mungu.

SEHEMU YA TANO: Yesu Alionyesha Huruma kwa Kuwafufua Wafu

Kifo ni tisho kwa kila mtu. Yesu alihuzunishwa na kifo kama mtu mwingine ye yote. Alilia baada ya kusikia kwamba Lazaro amekufa. Yesu alimpenda sana Lazaro. Alijua kwamba atamfufua lakini jambo hili halikumzuia kulia na kuhuzunika.

Je! wanawake Wakristo wanaweza kujifunza nini kulingana na mwito wa Yesu kwa kifo? Hawawezi kufufua wafu kama Yesu. Je! tunaweza kushiriki ujumbe wa matumaini? Ndio! Tunaweza kumwambia Martha maneno ya Yesu. Yesu ndiye ufufuo na uzima. Ye yote anaye mwamini ataishi tena ingawa atakufa. Tunapaswa kuomboleza na waliofiwa na kuwafariji jinsi Yesu alivyofanya.

Wale waliofiwa huwa hasa wanahitaji msaada wa chaklula na mavazi. Wanawake Wakristo wanapaswa kuwa wa kwanza kusaidia na kile walicho nacho. Tunaweza kusaidia kifedha kwa maneno yetu ya kufariji. Tunaweza hasa kukaa na wanaoomboleza, na kuwafariji kwa kuwa tu nao.

ulivyo navyo vyote na uwape maskini pesa utakazopata." Kijana huyu alienda zake akiwa na huzuni sana. Yesu alitambua shida kuu maishani mwake. Alipenda sana pesa kuliko Mungu.

Haimanishi ya kwamba Mungu anataka kila mtu auze alivyo navyo na awape wengine pesa alizo uzia. Lakini anataka awe wa kwanza katika maisha yetu. Aliwaambia wanafunzi wake kuwa ni vigumu kwa tajiri kuingia ufalme wa Mungu. Mungu anataka awe Bwana wa maisha ya kila mtu.

Hadithi hii inatuonyesha kuwa sio kila mtu tunaye mshuhudia atampokea Yesu. Kazi yetu si kuwashawishi. Kazi yetu ni kuwaambia habari za Yesu. Ni kazi ya Roho Mtakatifu kuwafunulia dhambi zao.

SEHEMU YA NNE: Mwanamke Msamaria

Sote tunakumbuka hadithi inayotuelezea jinsi Yesu alimshuhudia mwanamke Msamaria aliyekuja kuchota maji pale kisimani. Alikuwa mtu ambaye alikuja tu siku hiyo kuchota maji. Yesu hakuwa ameagana naye kwamba wakutane hapo. Lakini alikuwa tayari kuzungumza naye, mtu wa kabila lingine. Alikuwa tayari kumwambia habari za upendo wa Mungu.

Yesu alikutana na mwanamke huyu alipokuwa na hitaji. Alilinganisha hitaji lake la kiroho na lile la kimwili ili aweze kuelewa

vizuri. Alikuwa kuchota maji kwa hivyo alizungumzia juu ya maji ya uzima.

Yesu aliendelea kuzungumzia habari za Mungu wakati mwanamke huyu alipotaka kuzungumzia jambo lingine. Mwanamke huyu alitaka kuzungumzia juu ya "Kanisa" na jinsi ya kuabudu. Yesu alijua kwamba mambo haya anayotaka si muhimu. Jambo muhimu lilikuwa kwamba mwanamke huyu awe na ushirika na Mungu Baba.

Mwanamke huyu alipoamini alikimbia mbio kwenda kuwaambia rafiki zake na watu wengine wa kijiji chake. Yesu alikuwa tayari kuwaambia habari za Mungu.

Yesu hakuzuliwa na imani za kidesturi. Myahudi hakuruhusiwa kuzungumza na Wasamaria. Wala hawakutakiwa kusema na wanawake. Yesu alihusika sana na mtu mwenyewe kuliko mila na desturi.

KIONGOZI:

Tumesikia leo hadithi nne za watu waliokutana na Yesu. Wengi wao walimpokea Yesu kama Mwokozi. Mmoja hakumpokea. Tumejifunza kwamba Yesu ndiye aliyewaendea. Alikuwa tayari kuongea na watu wa kila aina. Hakungojea watu wamwendee, hata hivyo alisema nao iwapo walimjia. Alikuwa tayari kusema na watu ambao walipuuzwa au walio kemewa na watu wengine.

Je! ndivyo ilivyo nasi wanawake Wakristo? Je! tunawezaje kuchukua

Waliingia katika nyumba ya wanawake wawili makahaba. Nyumba hii ilikuwa ya matope. Ndani kulikuwa kuchafu sana. Mchungaji huyo na washiriki wa kanisa waliwaambia habari za upendo wa Yesu. Wanawake hawa walifurahi sana na wakatoa maisha yao kwa Yesu Kristo. Wakawaambia, "Tulifikiri kwamba hatungetembelewa na mtu ye yote kwa sababu tunaishi mahali pachafu sana. Zamani kulikuwa na kanisa hapa lakini liliondolewa kwa sababu kuna walevi na makahaba wengi hapa.

Yesu alisema kwamba nimekuja kuwaita wenye dhambi na si wenye haki. Tunapaswa kufuata mfano huu na tuwaendee watu po pote walipo. Ni lazima tuwaambie habari njema jinsi Yesu alivyofanya. Kumbuka kwamba kuna watu wengi ambao wanataka kusikia Neno la Mungu. Lakini wao wanajishughulisha na kazi zao wenyewe kama Mathayo. Hawana wakati wa kuja kanisani.

SEHEMU YA PILI: Yesu na Nikodemo

Nikodemo alikuwa mtu tofauti sana na Mathayo. Alikuwa kiongozi wa dini na Mfarisayo. Alijua mengi kuhusu Biblia lakini hakuwa ameokoka.

Nikodemo alitaka kujua mengi zaidi juu ya Yesu. Kwa hivyo, alimwendea Yesu usiku na kuanza kumwuliza maswali. Yesu akamwambia, "Ni lazima uzaliwe

mara ya pili." Aliendelea kuzungumza na Nikodemo mpaka Nikodemo akaanza kuelewa.

Alimwelezea jinsi Mungu alivyoupenda ulimwengu na akamtoa mwanawe afe ili ye yote amwaminiye asife bali awe na uzima wa milele. Yesu alisema kwamba shida ya watu wengi ni kwamba wanapenda sana giza kuliko nuru. Wanataka tu kuendelea na maovu wanayofanya.

Siku hizi pia kuna watu kama Nikodemo wanaweza kuwa makanisani mwetu. Ni watu wema, na wanaonekana kama Wakristo. Lakini hawajazaliwa mara ya pili. Pengine wana maswali. Sisi kama wanawake Wakristo tunapaswa kuwa tayari kuwaambia watu wa kanisa letu habari za imani yetu. Ikiwa mtu anakwenda kanisani kila Jumapili, haimanishi kwamba yeye ni Mkristo. Tunapaswa kuwa tayari kumwelezea habari za Mungu mtu ye yote anayetuuliza. Nasi tunapaswa kusoma Biblia zetu ili tuweze kujibu vizuri.

SEHEMU YA TATU: Yesu na Kijana Tajiri

Kijana mmoja tajiri alimwendea Yesu kumwuliza habari za uzima wa milele. Yesu alimwambia atii sheria alizopata katika Biblia. Kijana huyu alimjibu kwamba ametii amri hizo tangu utotoni. Lakini Yesu alijua moyo wa kijana huyu. Alijua kwamba yeye anapenda sana mali na fedha. Yesu alitaka kujua msimamo wake. Akamwambia, "Enenda ukauze

Ni desturi ya makabila mengi ya kiafrika kulia kwa sauti kwa muda mrefu. Watu wengine hujilazimisha kulia ili waonekane kuwa wanaomboleza. Ni jambo la kawaida kulia, lakini hatupaswi kulia kwa kusingizia. Wanawake Wakristo wanastahili kuwafundisha wengine kwamba haitasaidia kulia kwa sauti na kwa nuda mrefu. Maombi yetu yanapaswa kuwa kwamba muda wa kuomboleza na kuhuzunika kwa waliofiwa uwe mfupi.

KIONGOZI:

Tumezungumzia kwa kirefu fundisho la Yesu kuhusu huruma. Tumeguswa sana na jinsi alivyo

hurumia watu. Amekuwa mwalimu wetu. Ni jambo moja kufundishwa na jambo lingine kufuata mfano wa mwalimu. Kuna mambo mengi ya kuhuzunisha sana hapa Afrika ambayo hutufanya tujawe na huruma. Tumepewa mwito. Je! tutamwambia nini Bwana wetu wakati wa hukumu ya mwisho? Yesu anasema kwamba yale tunayo wafanyia walio wadogo huwa tunamfanyia. Je! tunamfanyia nini Yesu? Hapa Afrika huwa tunakutana na Yesu kwa njia mbali mbali akiwa amevalia aina tofauti ya mavazi. Je! huwa tunamtambua? Tumwombe Mungu atusaidie kuona mahitaji ya jamii zetu na hasa kuwasaidia wenye mahitaji.

Mpango wa Tatu

BWANA, TUFUNDISHE KUOMBA

Kilini Cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatiifu: Luka 11:1-13

Kifungu cha Kukumbuka: "Nami nawaambia, ombeni nanyi mtapewa, tafuteni, nanyi mtaona bisheni, nanyi mtafunguliwa."

Luka 11:9

KIONGOZI:

Wanafunzi wa Yesu walimwendea na kumwambia awafundishe jinsi ya kuomba. Walijua kwamba Yesu aliomba kila mara. Walimwona akiomba akiwa katika kundi na pia akiwa peke yake. Walijua kwamba aliamuka asubuhi na mapema kwenda kuomba. Walijua yeye aliomba kabla ya kufanya jambo lo lote muhimu. Walijua jinsi Yesu

alivyo mpenda Baba yake. Walijua yeye ni mwalimu mwema. Kwa hivyo walimwuliza Yesu awafundishe kuomba jinsi yeye mwenyewe alivyoomba.

Tutarudia leo baadhi ya mafundisho ya Yesu, yanayohusu maombi. Tutajifunza mfano wa ombi tunaota sala ya Bwana. Tuwe kama wanafunzi na tumwulize Yesu atufundishe jinsi ya kuomba.

SEHEMU YA KWANZA: Mfano wa Sala

Wengi wetu tunaweza kukariri mfano wa sala ambao Yesu alifundisha katika Mathayo 6. Hebu tusome pamoja sala hiyo: "Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yafinyike, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu."

Yesu hakutaka tuwe tunakariri tu sala hili kila mara. Alitupa ili atufundishe mambo muhimu kuhusu sala. Mambo yafuatayo ni yale ambayo tunaweza kujifunza kutoka kwa sala hii:

1) Ni lazima tuelekeze sala yetu kwa Mungu Baba. Hatuwaambi malaika au viumbe wengine wo wote. Tunapoomba huwa tunawasiliana na Mungu wa ulimwengu wote. Hilo ni wazo la ajabu!

2) Tunapaswa kwanza kumtukua Mungu tunapoomba. Mungu ni mtakatifu na anastahili sifa na ibada zetu.

3) Tunapaswa kumwambia Mungu mahitaji yetu. Mungu anajua mahitaji yetu, lakini ametuamuru tumwulize. Anataka tuwasiliane naye kama mama mzazi anavyotaka watoto wake wawasiliane naye.

4) Tunapaswa kumwomba Mungu msamaha. Sote tunajua kwamba

tumefanya dhambi. Tutaendelea kuwa na ushirika na Mungu ikiwa tutakiri na kutubu dhambi hizo na kuomba msamaha.

5) Tunapaswa kumwomba Mungu atuongoze. Mungu anataka ahusike katika mpango na uamuzi wetu. Yuko tayari kutuongoza ikiwa tutamsikiliza.

SEHEMU YA PILI: Maelezo Zaidi Kuhusu Sala

Yesu aliwaambia wanafunzi wake njia mbaya za kuomba kabla ya kuwapa mfano wa sala. Hebu sikiliza maneno yake kutoka Mathayo 6:5-6. "Tena msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amini, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini, na Baba yako aonaye sirini atakujaza."

Yesu hakusema kwamba si vizuri kuomba hadharani. Alikuwa akizungumzia kuhusu nia zetu. Tunapoomba huwa tunawasiliana na Mungu. Lakini kama tunataka kuwapendeza watu, basi na tutarajie kupata jibu kutoka kwao, na siyo kwa Mungu.

Yesu aliendelea kusema katika kifungu cha 7 kwamba: "Nanyi mkiwa katika kusali msipayuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya

Hebu tuibebe imani kama ngao ili tuweze kujikinga na mishale ya moto kutoka kwa Shetani. Tumwombe

Mungu aimarishe imani yetu. Tuwe na muda naye kila siku ili tuweze kumwamini zaidi.

Mpango wa Tisa

KUWAAMBIA WENGINE HABARI NJEMA

Kilini Cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatifu: Yohana 3:1-21

Kifungu Cha Kukumbuka: "Kwa kuwa mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea." Luka 19:10

KIONGOZI:

Tutasikia leo hadithi mbali mbali jinsi Yesu alivyowaambia watu habari njema ya wokovu. Kwa sasa kazi hii inajulikana kama kushuhudia. Kazi moja wapo muhimu ya Mkristo ni kuwaambia wengine habari za Yesu. Je! Yesu aliwaendeaje watu? Je! tunaweza kujifunza kutoka kwake jinsi ya kushuhudia?

SEHEMU YA KWANZA: Yesu na Mathayo

Yesu alikuwa akitembea siku moja na akakutana na Mathayo, aliyetoza ushuru watu wa Yerusalemu. Mathayo hakujua kwamba Yesu anakuja siku hiyo. Yeye alishughulika tu na kazi yake. Kazi ya mtoza ushuru ilikuwa kutoza ushuru zaidi ya kiwango kilichowekwa na serikali. Watoza ushuru hao walichukua pesa za ziada walizopata na wakawa matajiri sana. Ni vizuri kwamba Yesu hakuja kuhukumu watu.

Yesu alimpata Mathayo na akamwambia, "Nifuate." Mathayo alisimama na akamfuata.

Yesu alienda nyumbani kwa Mathayo na akashirikiana na watoza ushuru wengine bila kujali. Hata walikula pamoja. Baadhi ya mafarisayo waliona tendo hili nao hawakufurahi kamwe. Hawakuelewa kwamba Yesu alikuja kuokoa watu wote.

Mathayo alimfuata Yesu kwa sababu ya upendo mkuu aliomwona nao. Mathayo alitaka kuwa kama Yesu, ingawa alichukiwa sana na watu. Yesu hakujali yale yangesemwa na watu. Alijua kwamba kazi yake ilikuwa kuwaonyesha watu wote upendo wa Mungu.

Je! sisi kama Wakristo tunafuata mfano wa Yesu? Au Je! tunangojea watu waje katika makanisa yetu au katika mikutano ya injili?

Siku moja mchungaji na washiriki kadhaa walitembelea kijijini.

mmoja, lakini wakashindwa. Yesu aliwaambia kwamba hawana imani ya kutosha.

Ni lazima imani yetu ijaribiwe. Hivyo ndivyo tunavyokua. Jane na Bwanake Joel walimpenda sana Bwana. Walikuwa na watoto watatu. Joel alipata nafasi kwenda ng'ambo masomoni kwa miaka mitatu. Alikuwa mgonjwa na akafa mara tu alipomaliza na kukaribia kurudi nyumbani. Jane aliachwa peke yake. Hakuelewa kwa nini Mungu aliacha yatokee hivyo. Je! atawatunzaje watoto hawa watatu akiwa peke yake?

Siku moja Jane alisoma kifungu hiki cha Biblia, "Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno," (Yakobo 1:2-4). Jane alikuwa katika hali mbaya sana, lakini alijifunza kumsifu Mungu na kumwamini hata wakati wa shida.

SEHEMU YA NNE: Matokeo ya Imani na Kuamini

Imani katika Mungu ina nguvu. Miujiza mingi haikutoka pale Kapenaumu kwa sababu watu hawakumwamini Yesu. Yesu aliwaambia watu mara kwa mara kwamba, "Ikiwa tu mtaamini."

Maria na Jane walikuwa wakienda nyumbani wakati wa usiku. Gari

walilokuwemo liliharibika kabla ya kufika nyumbani na hivyo wakalazimika kutembea. Njia waliyofuata ilipita mwituni ambapo kulikuwa na wanyama wakali. Kulikuwa na giza kuu. Mawingu ya mvua yalifunika anga. Wanawake walilazimika kubeba tochi.

Maria na Jane waliogopa sana ingawa walikuwa Wakristo. Walipiga magoti njioni na kuomba. Walimwomba Mungu awalinde na kuwawezesha kufika nyumbani salama. Kulitokea ngurumo na radi mara tu walipoanza safari. Mwangaza wa radi uliwawezesha kuona njia na wakafika nyumbani salama bila hata kusikia mnyama yeyote. Miujiza itafanyika maishani mwetu ikiwa tunayo imani.

Imani huleta ushindi. Maria na Jane walipata ushindi wa safari yao. Daudi alimwamini Mungu na akawaletea Waisraeli ushindi kwa kumwua Goliati. Hannah alimzaa Samweli na watoto wengine baada ya kumwamini Mungu. Kiwete aliponywa kwa sababu rafiki zake walimwamini Yesu. Hizi ni baadhi tu za hadithi za imani zinazo patikana katika Biblia. Tusimame imara katika Bwana ili tuwe na hadithi za ushindi katika maisha yetu.

KIONGOZI:

"...Na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo ni imani yetu" (1 Yohana 5:4). Ni vizuri kujua kwamba imani inaweza kushinda shida zote za ulimwengu!

maneno yao kuwa mengi." Tunapo wasiliana na Mungu. Tunapaswa kuzungumza naye kana kwamba tunazungumza na mzee tunayempenda na kumheshimu. Hatupaswi kumpigia Mungu kelele ili atusikilize. Hatupaswi kumlazimisha afanye jinsi tunavyotaka. Ni lazima tukumbuke kuwa tunazungumza na Baba yetu

Ni lazima tuwe tayari kuwasamehe wengine tunapo mwomba Mungu msamaha. Mathayo 6:12 inasema, "Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu."

Tunastahili kuendelea kuomba bila kukata tamaa. Yesu alisimulia hadithi ya mtu ambaye alimwomba jirani yake chakula usiku wa manane baada ya kutembelewa na mgeni asiyemtarajia. "Nawaambia ya kwamba, ijapokuwa haondoki ampe kwa kuwa ni rafiki yake, lakini kwa vile asivyoacha kumwomba, ataondoka na kumpa kadiri ya haja yake." (Luka 11:8)

Tunaweza kuwa na hakika kwamba Mungu atajibu sala zetu kwa sababu yeye ni mwema. Baba mzazi hawezi kumpa mtoto wake nyoka ikiwa atamwomba samaki. Yesu akasema, "Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, Je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?"

SEHEMU YA NNE: Mfano wa Jinsi Yesu Alivyoomba - Yohana 17

Sura ya kumi na saba ya Yohana ina sala ndefu ambayo Yesu aliomba kabla ya kushikwa. Kuna mambo kadhaa ambayo tunaweza kujifunza kutoka kwa sala hii.

Kwanza, Yesu aliomba kana kwamba ana mazungumzo na Baba yake. Alimwambia Mungu kile alichofanya, jinsi alivyotimiza kazi ambayo Baba alimtuma kufanya. Alimwambia Mungu jinsi watu walivyo itikia. Je! tunapoomba huwa tunafanya mazungumzo na Mungu? Je! tunasikiliza itiko lake?

Pili, Yesu aliwaombea wafuasi wake. Aliwaombea wawe salama kwa sababu alijua majaribio magumu yanakuja mbele yao. Yesu hakuwaombea wajiepushe na shida, lakini na taabu hizo. Je! tunapoomba hukumbuka kuwaombea wengine au huwa tunajiombea tu sisi wenyewe?

Tatu, Yesu aliwaombea wale ambao wangemwamini kwa sababu ya ujumbe wa wanafunzi wake. Watu hao ni sisi! Yesu alikuombea wewe na mimi, hata kabla hatujazaliwa. Je! hukumbuka kuwaombea wasio Wakristo tunapo omba? Je! huwaombea kwamba waokoke na watambue furaha ya wokovu?

KIONGOZI

Tumejifunza leo mambo mengi kuhusu sala. Tumeona kwamba sala ilikuwa ya muhimu kwa Yesu. Tumejifunza jinsi Yesu mwenyewe

alivyoomba. Hebu turudie kwa kifupi yale tuliyojifunza kuhusu sala:

1. Yesu aliomba kila mara.
2. Sala haipaswi kuwa jambo la kumpendeza mwanadamu, bali kuzungumza na Mungu.
3. Hatuombi kwa kutumia maneno yasiyo na maana, bali tunazungumza yenye maana na Mungu.
4. Sala huelekezwa kwa Mungu tu.
5. Msifu Mungu kwanza, mshukuru kwa yale aliyokufanyia.

Mpango wa Nne

JINSI YA KUSHUGHULIKA MAJARIBU

Klini Cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatifu: Mathayo 4:1-11, 1 Yohana 2:15-17

Kifungu Cha Kukumbuka: "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili." 1 Wakorintho 10:13

KIONGOZI:

Tutajifunza katika mpango wa leo jinsi ya kushughulikia majaribu. Je! majaribu ni nini? Majaribu ni hali ya kumshawishi mtu afanye maovu. Biblia inatufundisha kwamba Shetani ndiye hupinga kusudi kuu la Mungu. Ndiye chanzo cha tamaa na matendo yote ambayo ni kinyume cha upendo mtakatifu wa Mungu.

Wakati mwingine watu huchanganyikiwa kati ya majaribu na

6. Mwombe Mungu mahitaji yako.
7. Mwombe Mungu msamaha.
8. Mwombe Mungu awalinde watu wengine na awaokoe.
10. Omba bila kukoma.
11. Wasamehe wengine.
12. Kumbuka, tunamwomba Mungu kwa sababu ni Baba mwema ambaye anatupenda na anataka kujibu maombi yetu.

jaribio. Mungu hatujaribu tufanye dhambi. Lakini hujaribu uaminifu wetu kwake. "Mtu ajaribiwapo, asiseme, Ninajaribiwa na Mungu, maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu," (Yakobo 1:13).

Tutaangalia leo katika sehemu tatu maishani mwetu ambazo Shetani hutumia kutushawishi tufanye dhambi. Shetani alitumia njia hizi tatu kumjaribu Adamu na Hawa

lakini tunaamini kwamba ni kuzuri na tunatamani sana kuwa huko.

SEHEMU YA PILI: Jinsi ya Kuanza Kuamini

Ni vigumu sana kumwamini mtu ambaye humjui wanafunzi walijifunza kumwamini Yesu kwa kuwa naye kila wakati. Yesu alituliza dhoruba walipokuwa naye. Walijua kwamba ni Mungu tu ambaye anaweza kutawala maumbile na walianza kutambua Yesu ni mtu wa aina ya kipekee. Baadaye, Yesu alitembea juu ya maji. Petro alikuwa tayari ameanza kumwamini Yesu na akatoka ndani ya mashua kwenda kumlaki Yesu. Lakini imani yake ilikuwa fupi. Petro aliacha kumwanguka Yesu na akaanza kuzama. "Ewe mwenyeImani haba!" Yesu akamwambia. Hakuwa akizungumzia juu ya wingi wa imani ya Petro, lakini jinsi ilivyokuwa ya muda mfupi. Ni lazima imani yetu idumu milele ikiwa imo ndani ya Mungu Mwenyezi.

Roho ndiye hutupatia imani. Mtu mwenye imani ni mnyenyekevu kwa sababu anajua kwamba hawezi kitu cho chote pasipo nguvu za Mungu.

Mtu huwa na imani anapomwamini Yesu Kristo. Ni lazima aamini kwamba Yeye ni mwana na Mungu na ana uwezo mkuu. Hakuna mwingine kama yeye.

Mungu ni mwaminifu. Anastahili kuwa chombo cha imani yetu. Watu kama Daudi walijitoa maishani kumwamini Mungu. Ndiyo sababu Daudi aliweza kumshinda simba,

dubu, na hata Goliati. Danieli alikuwa na imani kwamba Mungu atamwokoa kutoka katika tundu la simba. Musa aliamini kwamba Mungu atayatenganisha maji nao watapata njia. Mashujaa wote wa Imani ambao tumesoma katika Waebrania 11 walijua kwamba Mungu ni mkuu, mwenye uwezo, mwenye nguvu na mjua yote na ndiyo sababu walimwamini.

SEHEMU YA TATU: Kuijaribu Imani Yetu

Kiasi cha imani ambayo mtu anayo ndicho kipimo cha kuonyesha jinsi anavyo mfahamu Mungu. Biblia inatusihi tumwamini Mungu kabisa.

Ni lazima Mwalimu awape wanafunzi wake mtihani ikiwa anataka kujua kama kweli wanaelewa kile anacho fundisha. Mungu pia hujaribu imani yetu. Majaribio haya hutusaidia kufahamu jinsi tunavyomwamini Mungu na hutusaidia kumwamini zaidi. Wakati mwingine majaribio haya huwa magumu, lakini Mungu hutujaribu ili kuimarisha imani yetu kwake. Musa aliwaambia Waisraeli kwamba, "Aliye kulisha jangwani kwa mana, wasiyojua baba zako; apate kukutweza, apate kukujaribu, ili kukutendea mema mwisho wako" (Kumbukumbu La Torati 8:16).

Yesu aliyaruhusu matukio magumu yatendeke maishani mwa wanafunzi wake ili kujaribu imani yao. Wanafunzi walijaribu siku moja kufukuza pepo kutoka kwa kijana

IMANI NA KUAMINI

Kilini Cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatiifu: Waebrania 11

Kifungu Cha Kukumbuka: "Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; Kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao." (Waebrania 11:6)

KIONGOZI:

Yohana na babake walikuwa wakilisha ng'ombe katika shamba lao. Yohana alikuwa na miaka sita. Alipanda juu ya mti wenye matawi ya chini. Alipanda juu zaidi karibu futi sita. Babake alikuja karibu na mti huo. Yohana akamwambia kwa sauti, "Baba naweza kuruka kutoka hapa nilipo mpaka pale ulipo." Babake akamjibu, "Tafadhali usiruke utaanguka na utaumia sana. Unaweza kuvunjika mguu au mkono." Lakini Yohana hakumsikiliza. Aliruka huku akisema, "Baba, ona jinsi ninavyoruka."

Baba yake alinyosha mikono yake na kumyaka kabla ya kuanguka. "Nilijua kwamba utaninyaka" Yohana alisema huku akitabasamu. "Nilijua kwamba utaninyaka kwa sababu uko karibu."

Kijana huyu alikuwa na imani sana kwamba babake alimjali sana na hangemwacha aanguke. Alijua kwamba hako hatarini kwa kuwa baba yake yuko karibu.

SEHEMU YA KWANZA: Je! Imani na Kuamini ni Nini?

Maneno haya Imani na Kuamini yana maana sawa. Ni kuwa na matumaini kwa mtu au kitu fulani. Kwa mfano ninapo mwachia Susan mtoto wangu, huwa sina wasi wasi kwa sababu anapenda watoto. Atamtunza mwanangu kama kwamba ni wake mwenyewe. Kwa hivyo hata nikichelewa najua kwamba mwanangu yu salama.

Kulingana na Agano Jipya imani ni tendo la kukubali karama za Mungu. Ni kama tunavyoambiwa na kifungu cha kukumbuka cha leo, Imani ni kuamini kwamba Mungu ni Mungu na kwamba atawatuza wale wanao mtafuta.

Waebrania 11:1 inatuambia kwamba imani ni kinyume cha kuona. "Basi Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Hakuna mtu aliye hai ambaye amewahi kuona jinsi mbinguni kulivyo, lakini tunaamini kwamba siku moja tutaenda huko. Hatujui jinsi kulivyo au jinsi tutaishi huko,

(Mwanzo 3) na Yesu (Mathayo 4:1-11). Hizi ndizo njia tatu ambazo Shetani hutumia hata sasa bila kiwango. Tunaweza kusoma juu ya njia hizi katika 1 Yohana 2:16: tamaa ya mwili, tamaa ya macho na kiburi cha uzima (majivuno).

SEHEMU YA KWANZA: Tamaa ya Mwili

Tamaa ya mwili ni hali ambayo chanzo chake ni ndani ya miili yetu. Ukiwa na njaa hutamani kula ili ushibe. Uonapo kiu, hutaka kunywa maji au kinywaji baridi ili uondoe kiu hiyo. Ukiwa mgonjwa huenda kutibiwa ili upone. Si vibaya kwetu kutamani au kuhitaji kitufulani. Shida hutokea wakati tamaa yetu huwa kuu sana mpaka Shetani huitumia kutujaribu.

Cheruto ni mweka hazina wa mradi wa wanawake wa eneo lake. Wanawake wengine walimchangua kuwa mweka hazina kwa sababu wanamheshimu. Yeye ameokoka na ni mwaminifu.

Lakini, siku moja, kabla ya kufanya mtihani wake wa kidato cha nne, bintiye alifukuzwa shuleni kwa kuwa hajamaliza kulipa karo yake. Hangefanya mtihani kabla wazazi wake hawajalipa shilingi 2000/- zilizobakia. Hawakujua mtu ye yote ambaye wangemwomba pesa hizo. Mwalimu mkuu hakukubali sababu hiyo yao. Alisisitiza kwamba ni lazima walipe karo hiyo.

Wakati huo huo ambao Cheruto alikuwa akiwazia karo ya binti yake,

shilingi 2000/- za Mradi wa wanawake zililetwa. Cheruto alipozipata, wazo la kwanza lilikuwa kwenda kulipa karo ya bintiye. Hangeweka rekodi ya pesa hizo na hakuna ambaye angejua kwamba amezipokea.

Lakini Cheruto aliwaza tena mara hiyo hiyo. Alijua kwamba ingekuwa kosa kwake kama Mkristo kuchukua pesa hizo na Mungu angeudhika. Cheruto alisumbuka sana moyoni mwake kuhusu atakacho fanyia pesa hizo. Alikaa siku tatu bila kumwambia ye yote jambo hili. Alikuwa na hitaji kuu sana. Shetani alimnong'onezea kwamba pengine Mungu amemwacha. Kwani, alikuwa amekombea jambo hili kwa muda mrefu lakini bado hakufanikiwa.

Wakati huo huo ambao Cheruto alikuwa karibu aanguke majaribuni alikumbuka Mathayo 19:26, "Kwa wanadamu hilo haliwezekani bali kwa Mungu yote yanawezekana." Kisha akakumbuka tena Marko 9:23, "Yote yanawezekana kwake aaminiye." Alitubu mara moja na akaamua kuweka pesa hizo katika akiba ya mradi wa wanawake. Cheruto alishinda jaribu hilo. Siku hiyo hiyo baadaye Bwana alimgusa mwanamke mmoja aliyeokoka. Mwanamke huyu alimpa Cheruto shilingi 2000/- za kwenda kulipa karo ya bintiye. Bintiye alirudi shuleni siku iliyofuata.

Yesu alikuwa jangwani katikati ya mawe kwa muda wa siku arobaini usiku na mchana. Hakuwa

amemaliza siku zake za kufunga, na aliposikia njaa, shetani alimwambia ageuze mawe hayo yawe chakula. Yesu hakushindwa na jaribu la kuyafanya mawe kuwa mkate. Bali alikariri maandiko yaliyo katika Kumbukumbu la Torati 8:3, "Mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana."

Dada zangu wapendwa, tusiache tushindwe na majaribu. Kumbuka kwamba Mungu atatupa njia ya kuepuka kila jaribu.

SEHEMU YA PILI: Tamaa ya Macho

Shetani alipomjaribu Yesu, aliyafanya mawe yaonekane kuwa yanafaa kwa mkate. Shetani hutumia macho yetu kuona vitu vizuri na kuvitamani.

Jane alikuwa akimshuhudia Ann jinsi ya kuokoka. Ann akamwambia, "Unaona ile televisheni ya rangi? Ni nzuri sana ya kutazama. Hiyo ni ya dada yangu. Sina kama hiyo na sijatulua bila kuwa nayo. Sifanyi kazi kama dada yangu. Unawezaje kuniambia niokoke, hali sijatimiziwa mahitaji yangu? Nikiokoka, siwezi kudanganya ili niipate. Lakini kwa sasa, naweza kufanya jambo lo lote kuona kwamba jamaa yangu wameridhika."

Sisi kama Anna huwa tunafikiria kwamba vitu vingi ni vizuri navyo vinaweza kutufanya tufurahi. Pengine huwa hatuna pesa za kuvinunua, hali tunavitamani. Huwa tunatamani nguo mpya, saa, nyumba, televisheni,

video, mashamba, kuwa na pesa nyingi benki na vitu vingine vingi. Yohana wa kwanza 2:15 inasema, "Msipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akipenda dunia, kumpenda baba hakumu ndani yake." Kumbuka kwamba mambo haya yote yatapita, jinsi tunavyoambiwa katika kifungu cha 17, "Na dunia inapita pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele."

Dada zangu, tusitumie macho yetu kama vyombo vya kufanyia dhambi na shetani. Bali tumpinge naye atatoroka.

SEHEMU YA TATU: Kiburi au Majivuno

Shetani alimwambia Yesu kwamba atampa ulimwengu wote na utukufu wake ikiwa atamwacha Baba yake na kuwa wa Shetani. "Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia "Haya yote nitakupa ukianguka kunisujudia." (Mathayo 4:8-9). Yesu alimpinga na akasema: "Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, 'Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake!'" (Mathayo 4:10)

Kiburi na majivuno ni jambo la kawaida siku hizi. Kila mtu anataka kutambuliwa kuwa yeye ni muhimu sana. Siku hizi kote duniani, kuna vita vya wenyewe kwa wenyewe katika mataifa mengi. Watu fulani

Kisha akawaambia, "Fuatani mfano huu."

Ingawa Yesu alikuwa mfalme, alienda Yerusalemu akiwa amempanda punda na siyo farasi aliyetumiwa na wafalme wa kidunia. Tendo hili lilionyesha upole wake. Pengine, kama angekuwa duniani siku hizi angetumia baiskeli na si gari la Mercedes Benz.

Yesu hakujibu kamwe kukubali kuwa ai Kristo, alipatwa na wakati mgumu wala hakutumia mamlaka yake kujikinga. Hakulipiza kisasi alipodhihakiwa.

Yesu alituamuru kumfuata na kutii amri zake ikiwa tunampenda. Tunapaswa kujinyenyekeza naye atatuinua. Ni lazima tunyenyekee hata kama tunatoka katika kabila zuri au taifa.

Yesu alikataza majivuno ya kiroho. Alipinga tabia na mienendo ya Waandishi na mafarisayo, kwa kusema kwamba walifuata dini yao ili waonekane na watu. Je! umepata kuona viongozi wa kanisa ambao wanataka kujulikana na kuheshimiwa po pote waendapo? Hukaa kwenye viti vya mbele katika mikutano ili

waonekane na watu. Hutaka kuonekana watakatifu kuliko wengine. Hawataki watu wengine waongoze au washiriki katika ibada. Watu wenye kiburi hutaka kila wakati kuwa viongozi na kuhairisha upigaji kura wa kanisa ili waendelee kuongoza. Mwanamke mwenye kiburi atakataa kuwafundisha wengine yale anayojua ili aendelee kuongoza.

KIONGOZI:

Yesu huchukizwa sana na mifano hii yote ya kiburi. Tunastahili leo kuyachunguza maisha yetu na tuone pale ambapo tunatawaliwa na kiburi. Je! unawazuia wengine kumtumikia Bwana kwa sababu unafikiri kwamba wewe tu ndiye unayestahili? Tubu na uache dhambi yako. Kumbuka kwamba, "Tukiziungana dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote," (1 Yohana 1:9).

Fanya yaliyo ya haki na Bwana atakubariki. Tumwombe Mungu atusaidie kuwa wanyenyekevu. Tujifunze kuwa kama Yesu.

SEHEMU YA NNE: Matokeo ya Unyenyekevu

Sara ni mkurugenzi wa kampuni fulani. Anampenda Bwana. Mkubwa wake amejaribu mara nyingi kumshawishi wawe wanachukua pesa za kampuni na kuzitumia kama zao. Sara amemkataza kila wakati. Mwishowe mkubwa huyo aliamua Sara afutwe kazi. Mkubwa wake aliwaandea wenye kampuni hiyo na kumshitaki Sara kwa mambo ya uongo. Rafiki za Sara walimshauri kuwa amshitaki kortini kwa kuzusha uongo, lakini Sara alikataa. "Ninaamini kwamba Mungu ndiye aliyenipa cheo hiki. Atanirudisha kazini ikiwa anataka niendelea na kazi hii. Mungu ni ngome na mtetezi wangu. Atanipa kazi nyingine."

Sara alifutwa kazi. Alipata kazi nyingine nzuri baada ya muda mfupi. Kazi hii ilikuwa na mshahara mkubwa, faida nzuri, na alipewa gari, nyumba na kulipwa mafunzo zaidi. Sara alimsifu Mungu kwa uaminifu wake.

Biblia inatuambia kwamba unyenyekevu huleta utajiri na maisha marefu. "Thawabu ya unyenyekevu ambao ni kumcha Bwana ni utajiri na heshima, nayo ni uzima," (Mithali 22:4). Mungu huwatetea walio wanyenyekevu miyoni mwao. Alimlinda Ayubu wakati Shetani aliposema kwamba Ayubu alimpenda Mungu kwa sababu mkono wa Mungu ulikuwa juu yake. Alimlinda Musa wakati Haruni na Miriamu walipo msingizia mabaya. Mwanzo

12:3 inasema, "Musa alikuwa mtu mnyenyekevu, mnyenyekevu kuliko mtu yeyote ulimwengu."

Tunaona kwamba ni vyema kunyenyekea mbele za Mungu ili aweze kutuina. Yakobo anatuambia kwamba, "Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu." na "Jidhilini mbele za Bwana naye atawakuza," (Yakobo 4:6,10).

SEHEMU YA TANO: Mafundisho ya Yesu kuhusu Kiburi na Unyenyekevu

Yesu ndiye mfano halisi wa unyenyekevu. Aliacha utukufu wa mbinguni ambapo alikaa kwenye mkono wa kuume wa Mungu, na kuja kutukombo. Wafilipi 2:5-9 inasema, "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwa pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu;... alijinyenyekeza akawa mtiifu hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina."

Yesu alikuwa Mungu, lakini hakutaka aheshimiwe. Badala yake alijinyenyekeza kwa ajili ya mwanadamu. Alimtukuza Mungu kwa kila hali ya maisha yake. Yesu alionyesha unyenyekevu wake alipoosha miguu ya wanafunzi wake.

wanataka vyeo serekalini. Wananchi wasio na hatia wanateseka na pia kuuawa. Kuna vita kati ya mataifa. Makabila pia yanapigana vita. Hii ni kwa sababu Shetani anatawala mioyo ya watu wengi hapa duniani. Watu hupata vitu katika ufalme wake kwa kutumia nguvu.

Jambo hili limeingilia hata jamaa. Baadhi ya wake wanataka kutawala mambo yote ya nyumbani. Biblia inasema wazi kwamba mume ni kichwa cha nyumba (Waefeso 5:23). Mke anapochukua nafasi ya mume wake huwa anafanya dhambi mbele za Mungu. Wanawake wengi wenye nia ya kutawala nyumbani huamua kuwapa talaka waume zao. Hutoroka na watoto wote na kuanza kujitawala. Mwanamke mmoja alipanga na wakora kumwua mumewe ili achukue mali yote ya mumewe. Watu hawa walikuwa matajiri sana. Lakini walishikwa na polisi baada ya kumwua mumewe. Mke huyu alihukumwa kifo. Kwa hiyo kiburi na tamaa yake ilimgharimu vyote alivyokuwa navyo.

SEHEMU YA NNE: Jinsi ya Kushinda Majaribu.

Tunaweza kutiwa moyo kwa sababu tunajua Yesu Bwana wetu alijaribiwa lakini akamshinda Shetani. Tutapata ushindi baadaye na hata wakati wa majaribu. Hebu tufikirie baadhi ya njia ambazo tunaweza kushinda majaribu.

Kwanza kabisa, ni lazima tujue neno la Mungu. Yesu alijua

Maandiko. Aliyakariri mbele ya Shetani. Tunaweza kutumia Biblia kumshinda Shetani ikiwa tunafahamu inavyo sema. Hatutamfanyia Mungu dhambi ikiwa tumeliweka neno lake miyoni mwetu. (Zaburi 119:11).

Pili, ni lazima tuombe kila wakati. Dada yangu, ikiwa unahitaji kitu cho chote, omba. Je! unatamani kupata kitu fulani? Mwambie Bwana. Je! unao moyo mzito? Omba. Yakobo 4 inatuambia kwamba hatuna kitu kwa sababu hatujamwomba Bwana. Tunaomba bila kupata kwa sababu tunaomba na nia mbaya, kutumia jinsi tunavyotaka. Tunapaswa kumwomba Mungu afanye mapenzi yake tunapoomba. Mungu ameahidi katika 1 Yohana 5:11-15 kujibu maombi ambayo yanaombwa kulingana na mapenzi yake. Tuombe jinsi Yesu alivyo fundisha katika Mathayo 6:13 kwamba, "Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu."

Tatu, ni lazima tumjue adui yetu. Ni vigumu sana kupigana kama hujui adui yako. Adui wetu ni Shetani ambaye anajulikana pia kama mshawishi. Unapaswa kujua hila zake. Petro wa Kwanza 5:8 inasema kwamba, "Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka zunguka, akitafuta mtu ammeze."

Nne, mpinge Ibilisi. Petro wa Kwanza 5:9 inaendelea kusema, "Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani." Yesu alimwambia

Shetani kwamba, "Nenda zako, Shetani."

Tano, ujazwe na Roho Mtakatifu. Yesu aliongozwa na Roho kwenda nyikani. Adirweza kumshinda Shetani kwa kusaidiwa na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni mwalimu, kiongozi na mshauri. Yuko nasi diama na hutusaidia kumshinda Shetani. Ni lazima tuwe na nguvu za Roho Mtakatifu maishani mwetu kila wakati ikiwa tunataka kumshinda Shetani na majaribu.

KIONGOZI:

Tumeona katika mpango wa leo kwamba tunaweza kumshinda

Shetani. Kumbuka kwamba Wakristo wengine hupatwa na majaribu hayo hayo. Sio dhambi kujaribiwa. Ni dhambi wakati unapotenda kulingana na majaribu hayo.

Yakobo 1:12 inasema, "Heri mtu astahimiliye majaribu, kwa sababu akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaahidia wampendao."

Yesu hakukosa kamwe kumtegemea Mungu. Alikataa kukubaliana na mambo ya kujinufaisha yeye mwenyewe. Sisi kama wafuasi wake, tunaweza pia kushinda majaribu.

Mpango wa Tano

UHUSIANO WA YESU NA WATU

Kilini Cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatiifu: Yohana 15:11-17

Kifungu Cha Kukumbuka: "Ninyi mmekuwa rafiki zangu mkitenda niwaamuruyo," Johana 15:14

KIONGOZI:

Mojawapo ya shida kuu ambayo watu wanayo hapa duniani siyo utajiri, umaskini au ugonjwa. Shida kuu ni mtu kufahamu yeye ni wa jamaa ya aina fulani. Watu wanahitaji kujua kwamba kuna mtu anaye wajali. Hutaka kutambuliwa na watu fulani. Watu hutaka mtu wa kuwasikiliza na kuwapenda. Hutaka mtu wa kuwafaraji.

Yesu alijua shida ya upweke. Aliwaambia watu waje kwake naye angewapumzisha, angewapa amani, upendo, furaha na kutatua shida zao. Yesu alianza uhusiano na watu binafsi. Tutaona leo jinsi Yesu alivyohusiana na watu aina mbalimbali. Tujifunze kutoka kwake tunapojifunza somo hili ili nasi tufanye vivyo hivyo.

Kiburi huchukuliwa kuwa chanzo cha dhambi na kuanguka kwa mwanadamu. Mwanadamu alitaka kuwa kama Mungu akijua mema na mabaya. Shetani alimjaribu ili afuate kiburi chake na kula tunda alilokatazwa.

SEHEMU YA PILI: Matokeo ya Kiburi

Tunaona katika kifungu cha kukumbuka cha leo kwamba watu wenye kiburi au kutakabari huelekea kuangamia. Tafsiri nyingine ya Biblia inasema kwamba kiburi huleta maanguko. Uovu hauwezi kamwe kuzaa mema.

Adamu na Hawa walitaka kuwa kama Mungu ili wajue mema na mabaya. Walianguka kwa kujaribu kujitakia makuu. Kiburi cha Hamani kilimfanya ajifikirie tu yeye mwenyewe. Tunasoma katika kitabu cha Esta jinsi alivyotaka kila mtu amheshimu. Alimchukia Modekai kwa sababu Modekai hakumsujudia. Alifikiri kuwa yeye niwa muhimu kwa sababu malkia alikuwa amemualika nyumbani kwake. Alifikiri kwamba mfalme anaongea juu yake aliposema kwamba anataka kumtuza mtu fulani. Aliona aibu kubwa alipoambiwa kwamba asaidie kumtuza Modekai.

Mfalme Herode alisifiwa sana na watu baada ya kutoa hotuba. Watu walisema, "Huyu si mtu anayeongea, bali ni Mungu." Malaika wa Bwana alimwangusha Herode mara moja. Alikufa kwa sababu hakumheshimu Mungu (Matendo 12:20-23).

Hadithi hizi zote zinaonyesha kwamba majivuno hutangulia kuanguka au maangamizi. Kiburi huleta kifo, uharibifu na aibu. Mithali 11:2 inasema, "Kijapo Kiburi ndipo ijapo aibu; Bali hekima hukaa na wanyenyekevu." Kiburi ni dhambi mbele za Mungu. "Macho yenye kiburi, na moyo wa kutakabari, hata ukulima wa uovu, ni dhambi," (Mithali 21:4).

SEHEMU YA TATU: Unyenyekevu

"Akaingia nyumbani kwake akasema, Salamu uliyepewa Neema, Bwana yu pamoja nawe. Naye akafadhaika sana. Kwa ajili ya maneno yake akawaza moyoni, Salamu hii ni ya namna gani?" (Luka 1:28-29).

Unyenyekevu ni kuwa na kiasi au hali ya upole au usikivu. Ni Kinyume cha kiburi. Kwa mfano, wakati malaika alipomsalamia Maria, alishangaa moyoni mwake kwa nini malaika alimtokea na kumsalamia jinsi hiyo. Alijinyenyekeza. Lakini angejisifu kama angekuwa na kiburi. Bali yeye alimtukuza Bwana na kuomba mapenzi ya Mungu yatimizwe.

Mwanamke mnyenyekevu hajivuni wema au maadili ambayo hana. Hajisifu kamwe. Hajivunii hali yake. Hutambua upungufu wake na kumtukuza Mungu kwa yale aliyomfanyia maishani mwake.

KIONGOZI:

Tumejifunza katika mpango wa leo kuhusu upendo. Tunapaswa kupendana jinsi Kristo alivyotupenda. Pengine kuna mwanamke katika ushirika wenu ambaye huwezi kumpenda kwa sababu amekutendea jambo fulani.

Mpango wa Saba

MAJIVUNO NA UNYENYEKEVU

Kilini cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatifu; Luka 18:9-14

Kifungu Cha Kukumbuka: "Kiburi hutangulia uangamivu, Na roho yenye kutakabari hutangulia maanguko." Mithali 16:18

KIONGOZI:

Leo tutazungumzia juu ya kiburi na unyenyekevu tunapoendelea na masomo yetu ya kuwa kama Yesu. Fundisho kuu katika Biblia juu ya kiburi linapatikana katika maisha na maneno ya Yesu Kristo mwenyewe. Yesu alikataza kiburi cha ukabila cha Kiroho na cha kijamii. Aina hizi zote za kiburi zipo katika ulimwengu huu wa sasa. Hebu tujifunze kutoka kwa mfano wa Yesu wa kupinga kiburi na kuwa wanyenyekevu kama yeye.

SEHEMU YA KWANZA: Kiburi

Yohana alianza kujivuna baada ya kupandishwa cheo kutoka kwa ufagiaji na kuwa mtunza vifaa na hatimaye kuwa msimamizi wa bahari. Alitaka walio chini yake wamheshimu. Mwisho alitamani sana

Pengine kuna mtu katika kijiji chenu ambaye humpendi. Pengine mtu huyo ni jirani au mmoja wa jamaa yenu. Kiri dhambi hiyo mbele za Mungu. Mwoimbe kupitia kwa ombi la Roho Mtakatifu kumpenda mtu huyu kupitia kwako.

kuchukua cheo cha mkurugenzi wake. Alitaka kila mmoja amwite "Bwana mkubwa." Alianza kujisifu kwamba hivi karibuni atakuwa mkurugenzi wa kampuni hiyo. Huu ni mfano wa kiburi na majivuno. Kiburi maana yake, kujifikiria wewe mwenyewe kwa hali ya juu. Mtu anaweza kujiona yeye ni muhimu sana kuliko wengine kwa sababu ya karama yake, uwezo, mali, au mambo aliyoyafanya. Kiburi ni kujitakia sifa na utukufu ambao hasa ni wa Mungu. Shetani alifanya hivyo huko mbinguni. Siku hizo alikuwa akiitwa Lusifa. Aliona wivu kuona Mungu ndiye anayepata sifa na kuabudiwa. Hivyo ndivyo alivyoanguka. Mungu alimfukuza mbinguni pamoja na malaika wote walioungana naye katika uasi wake.

SEHEMU YA KWANZA: Yesu na Wanafunzi Wake

Biblia haituambii mengi kuhusu Yesu kabla ya kuanza huduma yake. Watu wa kwanza ambao tunaona Yesu akihusiana nao ni wanafunzi wake. Watu hawa ni wale ambao Yesu aliwaita kufanya kazi naye na kuendeleza kazi yake baada ya yeye kuondoka. Si rahisi kwa watu kukutana kwa mara ya kwanza na kuwa marafiki. Kwanza ni lazima mtu aonyeshe kujali mwenzake. Hivyo ndivyo alivyofanya Yesu.

Petro, Yakobo na Yohana walifanya kazi usiku kucha, bila kuvua samaki hata mmoja. Yesu baada ya kufundisha umati, alimwambia Petro atupe nyavu yake baharini. Mara walivua samaki wengi sana mpaka mashua yao ikaanza kuzama majini kwa sababu ya uzito. Yesu akamwambia Simoni Petro, "Usihofu, kuanzia leo utakuwa mvuvi wa watu." Petro, Yakobo na Yohana waliacha kila kitu na kumfuata Yesu baada ya kuleta mashua yao ufuoni mwa bahari.

Jambo la pili ambalo ni la muhimu kwa kuwepo uhusiano ni kujuana. Sisi hujua kwa kukaa pamoja. Huzungumzana pamoja kwa kushiriki mawazo, shida, ushindi na mambo yaliyotushinda. Hakuwezi kuwa na uhusiano mwema kama kuna masengenyo. Hii ndiyo sababu Yesu alikuwa na wanafunzi wake kwa muda wa miaka mitatu. Aliwafundisha akashiriki nao na kuwaambia habari za Ufalme wa

Mungu. Miujiza aliyofanya ili wafundisha kumwamini.

Wanafunzi walijifunza mambo mengi magumu kutoka kwa Yesu. Wafuasi wengine wengi waliacha kumfuata Yesu kwa sababu hawakuelewa wala kukubali mafundisho yake. Yesu aliwageukia wanafunzi wake na kuwauliza, "Jel ninyi nanyi mwataka kuondoka? Basi Simoni Petro akamjibu, Bwana! Twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele. Nasi tumesadiki tena tumejua ya kuwa wewe ndiwe Mtakatifu wa Mungu." (Yohana 6:67-68). Uhusiano wao ulikuwa imara sana na hakuna kitu ambacho kingeuvunja.

SEHEMU YA PILI: Yesu na Ulimwengu

Yesu alikuwa na uhusiano mkuu na ulimwengu ingawa haukumtambua. Hii ndiyo sababu aliacha utukufu wake wa mbinguni na kuja kuukomboa ulimwengu. Yohana 3:16 inasema, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele." Aliwapenda wote bila mapendeleo. Yesu hasa alikuwa na wenye dhambi, watoza ushuru, makahaba, matajiri, maskini na watu wa aina yote watoza ushuru walichukiwa sana na watu wengine kwa sababu walitoza ushuru mwingi kuliko ule uliohitajika na Serikali. Walijiwekea pesa ya juu. Watu walishangaa kwa nini Yesu alikula

pamoja na watu waliojulikana kama wenye dhambi. Yesu akawaambia, "Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea" (Luka 19:10).

Tunajua hadithi za wanawake ambao wamekuwa na waume wengi au wale ambao wamewahi kuwa makahaba. Huwa hatujui jinsi ya kufanya urafiki nao. Lakini Yesu aliacha shughuli zake na kwenda kushiriki upendo wa Mungu na makahaba. Je! hii inatonyesha nini sisi kama wanawake Wakristo? (Wape muda wa kujadiliana.)

Ndiyo tunapaswa kuwaendea watu hawa ambao wanadharauliwa na kuwaambia habari za upendo wa Mungu. Tunapaswa kuwatembelea wafanya kazi wa baa na kuwaambia habari za upendo wa Mungu. Hata makahaba nao wanastahili kusikia habari njema. Tunapaswa kujishughulisha na wanawake ambao hawajaridhika na ndoa zao na wanataka kuwanyanganya wake wengine waume zao. Waambie wanawake hawa habari za upendo wa Mungu. Watembelee na kuzungumza nao, lakini usifanye kama wao. Waonyeshe njia ya kweli, njia ya wokovu.

SEHEMU YA TATU: Yesu na Wakuu wa Dini

Mafarisayo na Masadukayo hawakumfuata Yesu kwa sababu ya kujifunza kwake, lakini kwa sababu walitaka kumtega na kumshika.

Walitaka wamshitaki kwa kuvunja sheria walitaka pia kumwua.

Yesu aliwapenda viongozi hawa ingawa alijua mioyo yao. Aliwaonyesha kwamba wako makosa. Hakuogopa uwezo, mamlaka na vyeo vyao. Yesu aliwaambia kwamba "Ole wenu, mafarisayo, kwa mwapenda kuketi mbele katika masinagogi na kusalimiwa masokoni. Ole wenu kwa kuwa mmefanana na makaburi yasiyo onekana, ambayo watu wapitao juu yake hawana habari nayo. Nanyi wana-sheria, ole wenu, kwa sababu mwawatwika watu mizigo isiyochukulika, wala ninyi wenyewe hamwigusi mizigo hiyo hata kwa kimoja cha vidole vyenu. Ole wenu, kwa kuwa mwajenga maziara ya manabii, na baba zenu ndio waliowaua." (Luka 11:43-47.)

Watu kama hawa wako katika vijiji vyetu. Watu wengi wanateswa, wanachukiwa, wengine wanapenda vyeo, wengine wanataka kutambuliwa na kadhalika.

Sisi kama wanawake Wakristo tunapaswa kujifunza kutoka kwa Kristo. Hakuficha makosa ya viongozi wa dini wa siku hizo. Aliwakemea akifikiri kwamba watabadili mienendo yao. Nasi tunapaswa kufanya hivyo. Tunapaswa kudhihirisha wazi makosa ya jamii yetu tunayoipenda. Unapaswa kumshauri kwa upendo mwanamke wa kanisa lako ambaye anatomia cheo chake kuwanyanyasa wengine. Usiogope mamlaka au cheo chake lakini mwonyeshe kosa lake.

"Wapenzi, ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana...tukipendana, Mungu hukaa ndani yetu, na pendo lake limekamilika ndani yetu." (1 Yohana 4:11-12).

Kwa hivyo, dada wapendwa katika Bwana hebu nasi tupendane tukifanya hivyo, watu watajua kwamba sisi ni wa Mungu. Susan, mwanamke Mkristo, alimpeleka rafiki yake Joy ambaye hajaokoka kwenye ushirika wa wanawake wa kanisa lake. Joy alipendezwa sana na jinsi wanawake hao walivyoonyesha upendo wao kwa wenzao. Hakuwa amehona upendo kama huu. Alipendezwa na jinsi wanawake hawa walivyo ambiana shida zao, ushindi wao na mawazo tofauti katika mkutano huo. Joy aliamua kuwa Mkristo kwa sababu ya upendo aliouna kati ya wanawake hawa.

Upendo wa Yesu ulijionyesha wenyewe jinsi alivyowahudumia wanadamu. Upendo wetu kama wanawake Wakristo ndiyo ishara kuu ya kuonyesha Ukristo wako.

Siku moja Wangechi alimwambia Mumbi kwamba, "Inaonekana kwamba sitaweza kamwe kumpenda Beatrice. Nimejaribu sana kumpenda, lakini naona dhidi ninavyo jaribu kumpenda, ndiyo ninavyo zidi kumchukia. Yeye hujifanya tu kuwa ni Mkristo."

Mumbi akamjibu, "Ikiwa huwezi kumpenda Beatrice, basi hakuna tofauti kati yako naye. Watu wengine

watajua yakuwa tu Wakristo ikiwa watatuona kuwa na upendo. Kumbuka kwamba Yesu hakuwapenda tu wale waliompanda na kumtendea mema. Aliwapenda hata wale ambao hawapendeki. Kwa mfano, alimwacha Yuda Iskariote awe mwanafunzi wake ingawa alijua atamsaliti. Hakuna mahali popote katika Biblia panaposema ya kuwa alimchukia au alimtendea tofauti na wanafunzi wengine. Kwa hivyo ningekushauri umwombe Mungu ombi hili. 'Mungu, najua unatupenda bila upendeleo. Umetuamuru tupendane. Nakiri mbele zako kwamba nilishindwa kumpenda Beatrice. Nisamehe dhambi hii. Nipe upendo wako ili nimpende. Mwone kupitia kwa macho yangu ili nami nimwone jinsi unavyomwona. Nitumie kumtendea yale unayotaka."

Wangechi alifanya jinsi Mumbi alivyomshauri. Alijifunza kuanzia siku hiyo kumpenda Beatrice. Nia na mawazo yake kwake yalibadilika. Aliweza kumshuhudia kwa mara ya kwanza. Beatrice aliweza baadaye kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wake. Wangechi aliona furaha kuu kwa sababu alijifunza kumpenda asiyePENDKA.

Dada yangu, hii ndiyo siri ya kumpenda yule ambaye hapendeki. Tumia imani. Mwombe Mungu awapende kupitia kwako. Atafanya hivyo kwa sababu yeye mwenyewe ni pendo. Kisha nawe utapata upendo wa kweli moyoni mwako.

chao. Gladys na Judy hawakumwona mamba aliyekuwa akiota jua kando ya mto huo. Mamba huyo alitingisha mkia wake na kumchapa Judy, na akaanguka mtoni. Mamba alijitosa majini na kuuma mguu wa Judy. Gladys alipoona hivyo alipiga mayowe na kumfuata mamba huyo bila kujali iwapo kuna mamba wengine au kama atazama majini. Aliushika mkono wa Judy, na kwa mkono mwingine akampinga mamba puani kwa kutumia kibuyu cha chuma alichokuwa nacho. Aliamua kwamba ni afadhali wote wafe kuliko kumwacha rafiki yake afe peke yake. Alipiga mayowe na kulia na kusema, "Ee Mungu, nisaidie."

Mamba hakuthubutu kumwacha Judy. Gladys alichoshwa sana na mvurutano huu. Mwishowe alichoka sana na kibuyu chake kikamponyoka. Mamba aliona kibuyu hicho na akafikiri kwamba pengine ni mtu mwingine. Mamba huyo aliua mguu wa Judy na kufuata kibuyu hicho. Gladys aliweza kumtoa Judy majini mamba huyo alipofuata kibuyu kile. Alikuwa amemwokoa rafiki yake kutoka kwa kifo. Mfano huu ni wa upendo halisi.

Tulisoma katika maandiko yetu ya leo kwamba, "Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki yake." Ndivyo alivyofanya Yesu. Yesu alitufia tulipokuwa tungali wenye dhambi. Kifo chake msalabani kilidhihirisha nguvu za upendo wa kweli. Yesu alijitoa kama dhabihu

pale Kalvari kumkomboa mwanadamu. Upendo wake hauna mipaka wala kikomo. Anapenda ulimwengu wote. Hajali kama tu weusi, weupe, maji ya kunde, wekundu au manjano. Hajali iwapo tu wanene, wembaba, wafupi au warefu. Hajali nchi, wala kabila au jamii tunamotoka. Hajali iwapo tu wanaume, wanawake au watoto. Alitufia sote na anatupenda sote.

Vivyo hivyo, sisi kama Wakristo tunapaswa kufuata mfano wa Kristo na tuwapende watu wote bila kujali dini au hali yao.

SEHEMU YA NNE: Yesu Anaamuru: Mpendane

Yesu aliwafundisha wale waliomfuata kwamba amri ya kupendana ndiyo ya muhimu zaidi. Wakati mwana sheria alipomwuliza amri iliyo kuu zaidi, Yesu alimwambia, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, ni hii Mpende jirani yako kama nafsi yako" (Mathayo 22:37-39).

Yesu aliwaagiza wanafunzi wake wapendane ili furaha yao ikamilike. Wanafunzi wake walitii amri hii. Wanafunzi wa Yesu walikaa pamoja wakashiriki vitu vyao vyote, wakaomba na kuwa na ushirika baada ya Yesu kufa na kufufuka. Mtume Yohana alijifunza umuhimu wa kupenda na akatusihi kwamba,

Wanawake Wakristo wanapaswa kuonyesha maisha ya Kristo katika uhusiano wao. Fanya yale ambayo Kristo aliwafanyia wengine. Wakemee wanapokosa.

(Swali la kujadiliwa: Je! unao wajibu wa kusema jambo ikiwa utamwona Mkristo mwenzako akitumia vibaya cheo na mamlaka yake?

SEHEMU YA NNE: Jamaa ya Yesu

Yesu hakuonyesha mapendeleo. Hakuichukua jamaa yake kuwa bora zaidi kuliko watu wengine. Tunaambiwa katika Marko 3:31-35 kuhusu wakati ambapo mama ya Yesu, ndugu na dada zake walimwendea alipokuwa akifundisha umati wa watu. Yesu akawajibu, "Mama yangu na ndugu zangu ni akina nani? Akawatazama wale walioketi wakimzunguka pande zote, akasema, Tazama mama yangu na ndugu zangu! kwa maana mtu ye yote atakayefanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu."

Mpango wa Sita

UPENDO

Kilini Cha Mwezi: MJIFUNZE KWANGU

Maandiko Matakatifu: Yohana 15:11-17

Kifungu Cha Kukumbuka: "Haya nawaamuru ninyi, mpate kupendana."

Yohana 15:17

Yesu hakufanya hivyo kuonyesha kwamba haipendi jamaa yake, lakini alitaka kutuonyesha kwamba kila mmoja ni wa muhimu kwake. Mtu anapozaliwa kiroho, hufanyika dada wa kiroho wa Yesu Kristo. Tunafanyika kuwa mama, ndugu na dada wa Yesu kwa kufanya mapenzi ya Mungu.

Je! hii inatuonyesha nini sisi kama wanawake Wakristo? (Wape muda wa kujibu.) Inatuonyesha kwamba tunapaswa kumpenda Mungu kwa moyo wetu wote, akili yetu yote na roho yetu yote. Tunapaswa kumshuhudia Kristo na kumletea watoto wa Kiroho na kuwakuza katika Kristo.

KIONGOZI:

Tumwombe Mungu atusaidie kutenda baadhi ya yale tuliyojifunza leo. Tuwe na uhusiano mwema na watu wote bila kuonyesha mapendeleo. Tusijitukuze sisi wenyewe, bali tunyenyekee mbele za Bwana na kufanya mapenzi yake. Hebu na tuwapelekee watu wote habari za Kristo.

KIONGOZI:

Tutajifunza kuhusu upendo katika mpango wa leo. Tutafikiria jinsi Yesu alivyofundisha kuhusu upendo na jinsi alivyowaonyesha watu upendo huu. Ni muhimu kwetu sisi kama wanawake Wakristo kujifunza na kufanya yale ambayo Yesu anatuamuru.

Tunaweza kujadiliana kwa kifupi swali hii, Je! upendo ni nini? (Wape muda wa kujadiliana.) Ndiyo, upendo ni upole, wema au kumwazia mema mtu mwingine. Najua kwamba wewe kama mama unawapenda sana watoto wako. Unataka kuwa karibu nao. Watoto wako hujisikia vivyo hivyo. Hata hutaka kukushika mkono au kukupapasa. Watoto wadogo hupenda kuvaa nguo za mama zao. Hii ni kwa sababu wanakupenda. Nawe pia umejitoe kuwashughulikia. Mtoto wako anapokuomba kitu, hufanya kila juhudi kuona kwamba umempatia. Mambo haya yote yanaonyesha upendo.

SEHEMU YA KWANZA: Yesu Alieleza Upendo wa Mungu

Tunamwona Yesu akimweleza Nikodemo upendo wa Mungu katika Yohana 3:1-21. Nikodemo alikuwa mwalimu wa sheria ya Mungu, lakini hakuelewa. Yesu alipomwambia kwamba ni lazima azaliwe mara ya pili. Yesu alieleza kwamba, "Mtu huzaliwa kimwili na wazazi, lakini huzaliwa kiroho kwa Roho Mtakatifu." Unaweza kuzaliwa kiroho kwa sababu ya upendo wa

Mungu. Yesu akaendelea kusema, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."

Kayume alikuwa Mkristo lakini jirani yake Joan hakuwa Mkristo. Joan alimdhahiki Kayume kila wakati alipomwona. Alimlaumu Kayume kwamba anajifikiria kuwa bora kuliko wengine kwa sababu yeye alisema anakwenda mbinguni. Tendo hili lilimkasirisha sana Kayume na akaamua kutokuwa rafiki wa Joan. Lakini usiku mmoja Joan alianza kujifikiria yeye mwenyewe na Mungu. Mara alitambua kwamba yeye ni mwenye dhambi. Aliamua kwenda kumtembelea Kayume na kumwuliza jinsi ya kuokoka. Kayume alifurahi sana kwa kuwa Mungu amejibu sala zake za wokovu wa Joan. Alimkaribisha Joan ndani na kumwelezea upendo wa Mungu, ingawa kulikuwa usiku sana. Joan alimpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wake usiku huo huo.

Kayume alifanya mapenzi ya Mungu. Alifuata mfano wa Yesu. Tunaona kwamba Yesu hakumpuuza Nikodemo hata ingawa alimwendea usiku. Aliweza kumweleza jinsi ya kuzaliwa mara ya pili. Hakumwambia kwamba, "Sasa ni usiku, nenda urudi kesho."

Hii inatufundisha kwamba hatupaswi kuwapuuza watu hata kama wanatujia saa gani kuuliza habari za wokovu. Tunapaswa

kumtambua Roho Mtakatifu na tuwe tayari kufundisha neno la Mungu wakati wote.

SEHEMU YA PILI: Yesu Anadhihirisha Upendo wa Mungu

Maria hupenda sana kutembelea na wajukuu zake huko kijijini. Huwaleta wote pamoja na kuwakumbatia. Kisha huwatemea mate kwenye mikono yao na kuwabariki kwa kusema: "Mungu wa babu zetu awalinde. Awe nanyi na awajalie watoto wengi. Naye awape ng'ombe wengi, mbuzi, kondoo na shamba. Nao wote wanao watakia mema wawe rafiki zenu kama kunao adui zenu wapate kuangamia." Hivi ndivyo babu na nyanya zetu walivyo wabariki watoto na wajukuu wao.

Yesu pia, alionyesha upendo wake kwa kuwabariki watoto. Yesu aliwakemea wanafunzi wake walipowakataza wakina mama kuwaleta watoto wao kwa Yesu. Akawaambia, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa kuwa watu kama hao ufalme wa Mungu ni wao." (Luka 18:16)

Enyi wanawake, ikiwa Mungu ametubariki na watoto, basi nasi tunapaswa kumrudishia Mungu. Tunapaswa kuwaruhusu kwenda shule ya Jumapili kujifunza neno la Mungu. Tunapaswa kuwafundisha habari za Mungu wanapokuwa nyumbani. Tunapaswa kuwaambia kwamba Mungu ni upendo naye anawapenda.

Rose ana watoto wenye umri wa miaka miwili na mitatu. Amewafundisha kuomba kabla ya kula na kabla ya kulala. Kila mtoto huwa na wakati wake. Kisha huimba wimbo huu; "Yesu nakupenda, kwa vile ulivyonipenda." Watoto hawa watamfuata Mungu hata watakapo kuwa watu wazima ikiwa Rose ataendelea kuwafundisha juu ya upendo wa Mungu.

Hatupaswi kuwafundisha tu watoto wetu peke yao. Kunao wazazi katika vijiji vyetu ambao hawamjui Bwana. Hawaoni umuhimu wa kuwapeleka watoto wao kwa masomo ya shule ya Jumapili. Sisi kama wanawake tunaweza kujitoe, hata kama ni mara moja kwa wiki, kuwakusanya watoto wa majirani na kuwaambia habari za upendo wa Mungu. Tunaweza kujitoe kufundisha shule ya Jumapili. Tunaweza kufundisha darasa la Wajumbe wa Yesu. Tukifanya mambo haya yote, tutakuwa tunafuata mfano wa Yesu nasi tutabarikiwa sana. Hata wale ambao hawana watoto wanaweza kufanya kazi hii, nao watapata furaha ya kuwa mama wa kiroho wa watu wengi.

SEHEMU YA TATU: Yesu Anadhihirisha Upendo Wake Kwetu Pale Msalabani.

Gladys na Judy walikuwa marafiki sana. Siku moja walienda mtoni kuteka maji. Mto wao ulikuwa na mamba wengi. Mtu alipaswa kujihadhari sana ili asiwe chakula